SUPA JACKPOT
TZS.1,104,580,144
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Msajili** wa Hazina ayaweka kitanzini mashirika yenye hoja nzito za CAG


UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Kutapakaa machimbo Butiama kunavyoharibu mazingira
Kinamama waathirika wa biashara wanyamapori, waliogeuka walinzi
HIMOFILIA
**Ugonjwa damu haigandi penye jeraha, anayeugua maradhi yake ya kudumu**

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Aprili 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581286
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Ajira mpya 43,500 zaja serikalini

UKURASA 2

**256,479**
Idadi ya walimu waliopo nchini. 171,920 wa shule za msingi na 84,559 wa sekondari

**433**
Uhakiki wa madai malimbikizo ya mishahara katika taasisi 433 kufanyika.

**150**
Taasisi 150 kukaguliwa malipo ya mishahara kuepuka 'watumishi hewa'.

**380,000**
Jumla ya kaya zitakazohakikiwa kama zina sifa kuendelea kunufaika na mpango wa TASAF

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2023/24 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC amjibu Gambo madai ya ufisadi

UKURASA 3




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi (kulia), akikabidhi sampuli ya ndege Boeing 767-300F kwa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Ndege Kenya (KQ), Allan Kilavuka kama kumbukumbu ya mwanzo wa mazungumzo ya ushirikiano wa kibiashara, baada ya kikao chao, Dar es Salaam hivi karibuni.

# Tume ya Hakijinai yabaini shida mpya watoto gerezani

UKURASA 2

MICHEZO VIUNGO YANGA SC WAMVURUGA NABI UK.24
KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Mchuuzi wa matunda aina ya matikiti-maji akitafuta wateja katika eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Tikiti moja liliuzwa kwa bei ya 5,000/. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Ajira 43,500 zaja serikalini

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imepanga kuajiri watumishi wapya 43,464 ili kukabiliana na uhaba uliopo, Bunge limearifiwa.

Mkakati huo ulibainishwa jana bungeni jijini hapa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene alipowasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Simbachawene alisema kuwa katika mwaka 2023/24, ofisi hiyo itashughulikia vibali vya ajira ili kujaza nafasi 43,464 zilizoidhinishwa katika ikama.

Ni mkakati unaobainishwa siku chache baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kubainisha kuwapo uhaba wa watumishi nchini kupitia ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6 mwaka huu.

CAG Charles Kichere anasema kuwa katika halmashauri 23 alizozikagua, alibaini kati ya walimu 28,677 wanaohitajika kwa shule za msingi na sekondari, kulikuwa na walimu 18,606 tu, hivyo kuwapo upungufu wa walimu 10,071 (asilimia 35).

Anasema hali hiyo inatokana na serikali kutoajiri idadi ya kutosha ya walimu, pia kutokuvutia walimu kwa kutoa mazingira bora ya kufundishia na maslahi ya kuvutia.

Ni hali inayokinzana na Mpango wa III wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22 hadi 2025/26 unaoelekeza uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika shule za msingi unatakiwa kuwa 1:50 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50) na kwa shule za sekondari ni 1:20 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 20) kufikia mwisho wa mwaka wa 2026.

"Kwa maoni yangu, upungufu wa walimu uliobainika katika mamlaka za serikali za mitaa 23 unaathiri kwa kiasi kikubwa ufaulu wa wanafunzi katika shule za umma.

"Ninapendekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Utumishi kutenga idadi ya kutosha ya walimu kwa shule zilizoathirika zaidi, kuongeza maslahi ya walimu, kulipa madeni na kutoa motisha kwa walimu," CAG Kichere anawasilisha hoja yake, ambayo Ofisi ya Rais - Utumishi inaonekana kuanza kuifanyia kazi.

Katika hotuba yake jana bungeni, Waziri Simbachawene alisema Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma (HR Assessment System) umewezesha kubaini idadi ya watumishi waliopo, kada zao, nafasi ya kazi, vituo vya kazi na majukumu wanayotekeleza.

Aliutaja ni mfumo uliowawezesha kubaini watumishi waliopo wa kada ya walimu 256,479. Kati yao, wa shule za msingi ni 171,920 na sekondari ni 84,559, akisema "mfumo pia umebaini mahitaji ya walimu kwa nchi nzima".

Waziri huyo alisema kwa mwaka ujao wa fedha watakagua orodha ya malipo ya mshahara katika taasisi 150 pamoja na kuhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara na kusahihisha taarifa zinazohusiana na masuala ya kiutumishi na mishahara ya watumishi kwa taasisi 433.

Vilevile, Simbachawene alisema Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) utahakiki na kutambua hali za ustawi wa maisha ya kaya za walengwa wa mpango zipatazo 380,000 iwapo zimeimarika kiuchumi kwa kutumia vigezo vya umaskini na utaratibu uliokubaliwa kitakwimu kwenye maeneo yote ya utekelezaji 186, pia kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 972,603 zinazokidhi vigezo vya mpango.

Waziri huyo pia alisema watauza viwanja 226 kati ya 326 vilivyopimwa eneo la USA RIVER jijini Arusha kupitia Watumishi Housing Investment (WHI).

"Serikali itayapa kipaumbele maeneo ya usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimalifedha. Bajeti hii itaiwezesha serikali kupandisha vyeo watumishi; ubadilishwaji wa kada au muundo wa utumishi; kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kutoa ajira mpya," Simbachawene alisema na kuliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.001 kwa ajili ya matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha.

**HOFU UPENDELEO**

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Kilwa, Ally Kasinge alisema wananchi wa Kilwa wanahisi katika ajira zinazotolewa na serikali, kuna viashiria vya ubaguzi, upendeleo na uonevu.

"Nikianza na 'case study' katika Halmashauri ya Kilwa, michakato kadhaa ya ajira imefanyika, karibu mitatu huko nyuma, lakini hata wale wenye sifa za msingi wanaotoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa wamekosa ajira.

"Hapa kuna jambo la kufanyia kazi serikalini, na nitoe wito au ushauri kwa serikali, hebu tukachunguze ajira tatu zilizofanywa kwa mfululizo katika Halmashauri ya Kilwa kama sheria zilizingatiwa na kama weledi ulitumika katika mchakato wa ajira," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko alisema taifa lolote linalohitaji kuendelea lazima liwe na usimamizi madhubuti wa rasilimaliwatu kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa ufanisi, akionya kuwa uhaba wa watumishi uliopo unatishia ufanisi katika utoaji wa huduma za kijamii na kutoa mianya ya ubadhirifu wa fedha za umma.

# Tume Hakijinai yabaini shida mpya watoto gerezani

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Kuangalia namna ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai imeelezwa makosa yanayoongoza kwa watoto wanaopelekwa mahabusu yanahusu kujamiiana wao kwa wao, mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Tume hiyo inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, ilielezwa hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea vituo vya polisi, mahakama ya watoto na magereza mkoani Dar es Salaam.

Meneja wa Mahabusu ya Watoto jijini Dar es Salaam, Darius Damas, aliiambia Tume hiyo kwamba, mashtaka yanayowakabili watoto ni mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha, ulawiti na ubakaji, matusi, dawa za kulevya na kukutwa na nyara za serikali.

"Kwa ujumla wanakabiliwa na makosa ya mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha; japokuwa na mengine yapo, katika makosa hayo wanakiri na kukutwa wametenda kweli," alisema Damas.

Alisema kosa lingine ni kuishi nchini bila kibali, ambalo linalowakuta watoto wanaosafirishwa kwa njia haramu, wakitokea nchi jirani.

"Malezi duni, single mothers (malezi ya mzazi mmoja) ndio changamoto kubwa inayosababisha haya yote. Makosa ya ubakaji na ulawiti kwa watoto yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na utandawazi, kwa kuona kwenye televisheni," alisema.

Pia, alisema sababu nyingine ni watoto kuangalia vipindi visivyofaa kwenye televisheni, kujiunga na makundi rika yasiyo na maadili, ukosefu wa mahitaji muhimu unaomsukuma kuiba na kujaribu mambo mapya kama ulawiti.

Aidha, alisema watoto wanaofikishwa mahabusu hiyo wanapata nafasi ya kurekebishwa tabia kwa kupewa ushauri na unasihi kutoka kwa maofisa ustawi wa jamii, michezo na burudani, kufundishwa ufundi stadi na kazi za mikono pamoja na elimu ya msingi kwa watu wazima, kwa walio na umri wa zaidi ya miaka 14.

Hata hivyo, alisema kituo hicho kinakabiliwa na uchakavu mkubwa wa miundombinu, uhaba wa vitendea kazi kama gari na bajeti ndogo ikilinganishwa na mahitaji.

Katika Kituo Jumuishi cha Mahakama, kilichopo wilayani Temeke, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Watoto Kisutu, Vicky Mwaikambo, aliiambia Tume kwamba kati ya kesi zinazoongoza kupokewa kwenye mahakama hiyo, ni zinazohusu watoto kujamiiana wao kwa wao.

"Katika mashauri 852 yaliyoamuliwa ni 750 kwa kipindi cha mwaka jana, kati ya hayo takribani 700 yalihusu madai na mengine jinai, hadi sasa kwa mwaka huu tumepokea mashauri 238 ambayo kati ya hayo, 208 ni madai na jinai 30 jinai," alisema.

"Makosa mengi ya kujamiiana watoto kwa watoto, kwa sababu hapa hatupokei shauri la watu wazima. Ila changamoto ni walioathiriwa kutokubaliana na uamuzi, kwa sababu makosa wanayofanya ni makubwa kuliko adhabu iliyopo kisheria.

Hakimu huyo alishauri kuwapo gereza maalumu kwa ajili ya watoto waliokutwa na makosa kisheria, hasa kwa watenda kosa wa umri kuanzia miaka 15 hadi 17.

"Kwa watoto ambao ni waathiriwa wa vitendo hivyo, wapo maofisa ustawi wa jamii ambao wanawapa ushauri nasaha. Ukomo wa kesi makamama ya watoto ni miezi sita. Kwa mwaka 2022 kesi za jinai zilikuwa 132," alisema Hakimu Mwaikambo.

Jaji Othman Chande, akipokea maoni hayo alisema bado sheria zilizopo nchini ikiwamo ya Mtoto ya Mwaka 2009 na mapitio yake imetokana na Sheria ya Mtoto Kimataifa na utekelezaji wake kuwa katika mazingira ya nchi husika.

Tume hiyo pia ilitembelea gereza la Segerea, Ukonga, Chuo cha Taaluma ya Urekebu cha Jeshi la Magereza Ukonga, Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, vituo vya polisi vya Buguruni, Mabatini, Kawe na Mahakama ya Watoto Temeke.

Tume ilipokuwa Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Mkuu wa Chuo hicho, Lazaro Mambosasa, alisema kinachofanyika sasa ni kukipanua na kuboresha mitaala ili kuendana na dunia ya sasa na wapo kwenye hatua za kuanzisha kituo cha utafiti ili iwe rahisi kufanya maboresho yanayohitajika kwa wakati.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Restuta James**

HABARI KITAIFA

# DC amjibu Gambo madai ya ufisadi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NI mnyukano wa kisiasa. Hivyo ndivyo inaweza kuelezwa kutokana na mvutano ulioibuka kati ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtehengerwa, na Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo. Hiyo ni baada ya Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani hapa kumuonya Gambo na kumtaka kuacha kufanya siasa za kuwatuhumu viongozi kwa tuhuma za ufisadi.

Katika onyo lake, Mtehengerwa amemtaka mbunge huyo kuacha kufanya siasa za maji taka na utoto kwa kutafuta huruma ya wananchi kwa kuwatuhumu viongozi kwa mambo yasiyo ya kweli kwa kuwa wanasimamia utekelezaji wa mipango ya jiji la Arusha.

Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari walipotaka kujua msimamo wake baada ya Gambo kuchangia hoja bungeni Aprili 17, mwaka huu, akielezea ubadhilifu wa fedha za umma katika jiji la Arusha.

Mkuu huyo wa wilaya alisema mbunge huyo hajui wajibu wake na anaendesha siasa za kitoto za kuchafua viongozi kwa tuhuma ambazo si za kweli.

"Nadhani hapa kuna tatizo. Watu ambao wamepewa dhamana ya kusimamia halmashauri ni madiwani na mbunge mwenyewe lakini hawajui dhamana yao. Kama waliona kuna mambo hayaendi vizuri, wangekuwa wa kwanza kuzuia na kuchukua hatua za awali ila kinachofanyika hapa ni siasa za kitoto," alisema Mtehengerwa .

pia, alisema kitendo anachokifanya mbunge huyo ni kutafuta njia ya kutokea na kusaka umaarufu usio na tija na watu wenye upeo mkubwa na uelewa wanaweza kumhoji alikuwa wapi wakati mambo hayo yakitokea au na yeye ni sehemu ya mpango huo.

"Kama haya anayosema yako na wao ni watu waliopewa mamlaka ya kusimamia halmashauri akiwamo Mbunge na madiwani basi hawakutimiza wajibu wao basi hawatoshi kuendelea kuwa viongozi wanaosimamia jiji letu.

"Sisi kama wilaya tunawajibu wa kuingilia pale tunapoona akili za halmashauri zimefikia ukomo na mambo hayaendi na nilipoingia madarakani nilizungukia miradi yote na kuwaita madiwani wote na kutoa maelekezo," alisema.

Pia alisema, alisema mambo yanayodaiwa na mbunge huyo, yalifanyika mwaka mmoja au miwili iliyopita na mengine yako mahakamani na mamlaka zingine zinaendelea na uchunguzi.

Jumatatu wiki hii, akiwa bungeni, Gambo alitoa tuhuma kuhusu mambo kadhaa ukiwamo ufisadi katika Jiji la Arusha, akidai tatizo kubwa ni ubadhilifu na usimamizi mbovu wa fedha za halmashauri hiyo.

Alitolea mfano baadhi ya tuhuma ukiwamo ujenzi wa jengo la utawala lenye urefu wa ghorofa sita huku akisema halmashauri imetafuta fundi mjenzi (rafiki yao) bila kutangaza tenda, taratibu za ununuzi hazikufuatwa na kumpatia Sh, milioni 199.7 kinyume cha utaratibu.

# Ndege ya mizigo ATCL kuchochea ushirikiano Tanzania na Kenya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ndege Kenya (KQ) inakusudia kuingia makubaliano na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa kampuni hizo.

Mtendaji Mkuu wa KQ, Allan Kilavuka na ujumbe wake, wamesema hayo wakati wa kikao cha awali na viongozi wa ATCL akiwamo Mtendaji Mkuu Mhandisi Ladislaus Matindi.

Akifafanua kwenye kikao hicho, Kilavuka alisema wamelazimika kufanya hivyo kutokana na uwapo wa maeneo mengi ambayo kampuni hizo zinaweza kushirikiana ikiwamo eneo la usafirishaji mizigo.

Alisema kuwa Kenya ni kituo cha usafirishaji mizigo katika Bara la Afrika kwa mizigo waliyonayo wanaweza kuingia makubaliano na Tanzania kuhakikisha ndege ya mizigo Boeing 767-300 yenye uwezo wa kubeba tani 54 kwa mara moja, inatumika kikamilifu.

"Hivi karibuni Tanzania itapokea ndege yake ya mizigo ambayo itaweza kutatua changamoto ya usafirishaji mizigo kwa kiwango kikubwa. Sisi tunaamini tunaweza kushirikiana kwenye eneo hili," alisema Kilavula.

Kuhusu abiria, alisema kampuni hizo zinaweza kushirikiana kuwasafirisha kwa kuzingatia misingi yenye kunufaisha pande zote mbili.

"Kupitia ndege tulizonazo, vifaa na wataalamu wetu wakitumika ipasavyo tutaongeza thamani na kupunguza gharama za uendeshaji wa ATCL na KQ. Uwapo wa ndege ya Boeing 787- 8 (Dreamliner) na ujio wa ndege ya mizigo Boeing 767- 300F zinafungua fursa zaidi za kibiashara, alisema Kilavula.

Mhandisi Matindi alisema kikao hicho kimeangalia masuala yatakayosaidia ustawi wa kampuni hizo na nchi zao kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya soko duniani. Alitaja maeneo yanayokusudiwa kushirikiana ni pamoja na kubadilishana wataalamu, kuendesha mafunzo kwa vitendo pasipo kutegemea nchi za mbali na usafirishaji wa mizigo, ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa kampuni hizo.

"Soko la Afrika peke yake ni kubwa sana na linahitaji ushirikiano katika kulifikia hususani huduma ya kusafirisha abiria na mizigo. Mahitaji mengine ni pamoja na mafunzo kwa vitendo suala linalolazimu kusafirisha wataalamu kwenda nchi za Ulaya kwa ajili ya mafunzo ya siku mbili au tatu. Iwapo elimu hii inaweza kupatikana nchi jirani, itakuwa bora zaidi ili kuinua uwezo wa kampuni hizo mbili na kuleta tija zaidi kwa jamii inayowazunguka," alifafanua.





NEXT RECOVERY TANZANIA LIMITED

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu, **STANDARD CHARTERED BANK TANZANIA LIMITED,** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya Mdaiwa wa benki hiyo kama ilivyoorodheshwa katika jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kama ilivyoainishwa hapo chini;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE, MUDA NA MAHALI |
|---|---|---|---|
| 01 | EKARUA NEMES MAKOI T/A EKARUWA GENERAL SUPPLIERS | KIWANJA NA.1289, KITALU B, UBUNGO KIBANGU, DAR ES SALAAM, L.O NO. 352089, HATI NA.85482 YENYE JINA LA EKARUA NEMES MAKOI | Mnada utafanyika Alhamisi, Mei 11, 2023 kuanzia saa 4.00 Asubuhi mahali nyumba ilipo. |

VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA

1. Dhamana/Nyumba itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
2. Mnunuzi atakayeibuka mshindi atatakiwa kufanya malipo ya 25% ya bei ya ushindi mara tu baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% kulipwa ndani ya siku kumi na nne (14) tokea siku ya mnada. Kushindwa kufanya malipo kikamilifu kama ilivyoelekezwa malipo ya awali yatataifishwa na mnada utarudiwa.
3. Gharama zote za kubadilisha hati umiliki, kutwaa nyumba/kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakua za mnunuzi.

Mawasiliano piga Simu Namba: **0713262400, 0783516394, 0717425708**



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax akitoa taarifa Bungeni, jijini Dodoma jana, kuhusu hali ya amani na usalama nchini Sudan. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Msajili Hazina ayaweka kitanzini mashirika yenye hoja nzito za CAG

**Na Mary Geofrey**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, ameyaagiza mashirika na taasisi za umma, kujibu kwa wakati na kutekelezwa na kufungwa kwa hoja zote za ukaguzi za ndani na za nje zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mchechu alitoa agizo hilo jana katika mkutano wake na wenyeviti wa bodi, watendaji na wakuu wa taasisi na mashirika ya umma na wakala za serikali jana, jijini Dar es Salaam.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni 'Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kuelekea Uwekezaji Wenye Tija kwa Taifa'.

Alisema mashirika mengi yamefanya vizuri kupitia ripoti ya CAG isipokuwa kumekuwa na kasoro ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi.

"Yasemeeni mashirika, taasisi za umma hata baada ya kufanyiwa ukaguzi na CAG akishasaini mnaweza kuzungumza tu. Msikae kimya, ukikaa kimya na kuna mazuri ambayo yamefanyika, jamii haiwezi kufahamu isipokuwa upungufu unaobainika kwenye ripoti ya mwisho ya CAG" alisema.

Mchechu alibainisha kuwa baadhi ya hoja zilizojitokeza kwenye ukaguzi wa ndani na nje wa mashirika na taasisi za umma ni utendaji dhaifu wa kifedha inayosababisha mashirika kuendelea kupata hasara, kupungua kwa mapato ikilinganishwa na mwenendo wa matumizi.

"Hasara hii kwa kiasi kikubwa inachangiwa zaidi na utendaji duni, ukosefu wa vyanzo vya kutosha na imara vya mapato na udhaifu katika usimamizi wa matumizi na mapato, ufanisi mdogo katika kuimarisha mazingira ya biashara, kuchelewa kukamilika kwa miradi, kuchelewa kulipa hati za madai na hivyo kusababisha kulipa riba kubwa za adhabu," alisema.

Pia alisema sababu zingine ni usimamizi usiokidhi wa matumizi; ulipaji wa fidia usio na tija kutokana na kusitishwa kwa mkataba bila kufuata utaratibu, kuchelewa kulipa madeni na kusababisha malimbikizo ya riba na kiwango kidogo cha ulipaji wa wadai.

Alitaja pia udhaifu katika udhibiti wa ndani, rasilimali watu na mifumo ya utawala kuwa ni kutokuwapo kwa sera ya udhibiti wa udanganyifu na taratibu za kuzuia vihatarishi katika mashirika na kutokuwasilisha makato ya kisheria.

Mchechu alisema pia kuna upungufu katika usimamizi wa mapato na bajeti ambao umesababisha kukusanya mapato nje ya mfumo wa GePG, ukusanyaji hafifu wa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya mashirika, taasisi zinazotoa mikopo kutokuwa na mifumo thabiti ya ufuatiliaji na usimamizi wa mikopo.

Eneo lingine, kwa mujibu wa Mchechu ni udhaifu katika usimamizi wa ununuzi na mikataba; kuwa na madeni makubwa ambako juhudi zisizotosheleza za ukusanyaji wa madeni na changamoto za mikataba ambazo zinashindikana kutatuliwa.

"Hoja za ukaguzi kutotekelezwa kwa muda mrefu na nyingine kujirudiarudia, taasisi kutokutekeleza hoja za ukaguzi kwa muda mrefu na baadhi ya hoja kubwa na za msingi kujirudia kila mwaka," alisema Mchechu.

Pia alisema kuna usimamizi wa masuala ya kodi, uwekezaji katika mashirika ya umma na kusababisha vikwazo katika kuwapa motisha na vivutio wawekezaji wa kimkakati na usimamizi na matumizi duni ya tafiti na teknolojia.

Msajili pia alisema utendaji hafifu wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kuwa na upungufu wa maji katika mamlaka za maji, kiwango kisichoridhisha cha urejeshaji wa madeni, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maji.

**MAAGIZO YA RAIS**

Mchechu alisema ofisi yake inafanyia kazi maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuzichukulia hatua taasisi na mashirika ya umma ambayo yanajiendesha kwa hasara ikiwamo kuyafuta.

"Tunaendelea kufanyia kazi maagizo ya Rais. Tuko katika hatua nzuri na tutafanya wasilisho muda si mrefu," alisema.

Kuhusu mashirika na taasisi ambazo zilikuwa zinatoa gawio na kupitia ripoti ya CAG lakini yalibainika hayapati faida, alisema wanaendelea kufanyia kazi kuangalia kwa nini hayapati faida na huenda changamoto ni mitaji.

Alisema wengine hawana uongozi imara na wanawakumbusha kujirebebisha na kama hawatabadilika watafanya mabadiliko.

"Suala la Rais kufanya mabadiliko ni jambo ambalo linatekelezeka na lipo 'serious' (makini) na yeye (Rais Samia) yuko 'serious'. Kama mtu hajajipanga vizuri, kuna Watanzania wengine wanaweza kuendesha mashirika hayo," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Meja Jenerali Michael Isamuhyo, akitoa shukrani kwa niaba ya washiriki hao, alisema watafanyia kazi maagizo hayo na kuanza kuyatekeleza kama ambavyo inatakiwa na ofisi ya msajili wa hazina.

# Tanzania yatangaza kuwaondoa raia wake Sudan kisa machafuko

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

TANZANIA imetangaza kuwaondoa raia wake 210 walioko Sudan kutokana na kuzuka mapigano kati vikosi vya serikali na vikosi vya usaidizi wa jeshi katika mji mkuu wa nchi hiyo, Khartoum, na maeneo mengine.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, akiwasilisha Bungeni jijini hapa jana, taarifa kuhusu hali ya amani na usalama nchini Sudan, alisema kati ya Watanzania watakaorejeshwa nyumbani, 171 ni wanafunzi walioko nchini humo kwa masomo na wengine ni maofisa ubalozi na raia.

Kwa mujibu wa Waziri Tax, hadi sasa hakuna Mtanzania aliyeripotiwa kuathiriwa na mapigano hayo, huku akiwahakikishia Watanzania kuwa serikali inachukua hatua stahiki kwa kushirikiana na nchi jirani, jumuiya za kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa ili kuhakikisha Watanzania walioko nchini humo na raia wengine wanakuwa salama. Mapigano hayo yalizuka Aprili 15, mwaka huu, yakihusisha vikosi vya Jeshi la Ulinzi la Sudan (SAF) na vikosi vya usaidizi wa jeshi (RSF).

"Serikali inaendelea kufuatilia na kuandaa mipango ya kuwachua raia wa Tanzania kadri itakavyohitajika. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa mapigano hayo yamesababisha vifo 185, majeruhi zaidi ya 1,000 na uharibifu wa mali, ikiwa ni pamoja na ndege. Aidha, mapigano hayo yamechangia kurudisha nyuma jitihada zinazoendelea za kutafuta amani nchini Sudan," alisema.

"Tanzania inasikitishwa na hali ya kuzorota kwa amani na usalama na imeendelea kufuatilia hali hiyo. Kama Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, Tanzania inaunga mkono tamko lililotolewa na Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika katika mkutano wake uliofanyika tarehe 16 Aprili, 2023 kulaani mapigano yanayoendelea nchini Sudan na inatoa wito kwa pande zote mbili katika mgogoro huo, kusitisha mapigano yanayoendelea," alisisitiza.

Kutokana na mapigano hayo, Waziri Tax aliliambia Bunge kuwa Tanzania inazitaka pande mbili zinazohasimiana kutatua mgogoro huo kwa njia ya amani huku zikihakikisha mahitaji ya kibinadamu, usalama na ustawi wa raia wa Sudan na raia toka nchi zingine.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na Ubalozi wetu uliopo Khartoum, ili kujua hali inavyoendelea.

"Juhudi hizi zimewezesha mapigano kusitishwa kwa saa 24 kuanzia jana tarehe 18 Aprili, 2023 saa 10:00 jioni ili kutoa fursa za mahitaji ya kibinadamu. Aidha, kutokana na juhudi hizi, uko mwelekeo wa kusitisha mapigano na kuruhusu njia za kutatua mgogoro huu kwa amani.

"Serikali, inatoa pole kwa wananchi wa Sudan na raia wengine na wote walioathirika na kuzorota kwa hali ya amani nchini humo kwa namna moja au nyingine. Tunaendelea kuzitaka pande zote mbili zisitishe mapigano na kurudi kwenye meza ya mazungumzo kwa ustawi wa Sudan, Afrika na dunia kwa ujumla," alisema.

# Mufti awataka Waislamu kuziba nyufa, kuendeleza mshikamano

**Na Mwandishi Wetu**

MUFTI Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir Bin Ali, amesema kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni cha kufanya marekebisho na kuziba nyufa katika maisha ya binadamu.

Pia amesisitiza mshikamano miongoni mwa wananchi ambao aliwataka kuendelea kuwa pamoja kama taifa imara.

Aliyasema hayo juzi katika Iftar iliyoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB), kwa ajili ya wateja na washirika wake wa kibiashara pamoja na wadau wengine ikiwa ni mwendelezo wa utamaduni wa taasisi hiyo kushirikiana na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

"Lengo la Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kuhakikisha wanadamu tunazidi kumcha Mwenyezi Mungu kwa namna mbalimbali kama wenzetu walivyofanya leo kupitia Iftar hii," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mufti, Shekhe Walid Alhad Omar Kawambwa aliishukuru TCB kwa kuandaa futari hiyo akisema ni ishara ya upendo na ushirikiano mkubwa na wa kizalendo iliyonayo benki hiyo kwa Watanzania.

Shekhe Kawambwa alisema kitendo hicho pia kinaendana na mafundisho ya dini ya kiislamu na maelekezo ya Mwenyezi Mungu ya ukarimu, upendo na ushirikiano hasa wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Shekhe Kawambwa ambaye ni Imam wa Msikiti wa Kichangani, Magomeni Mapipa pia aliwaasa Waiislamu na Watanzania wote kwa ujumla kuzingatia mafundisho ya Mtume Muhammad (SAW) hasa kipindi hiki cha Mfungo wa Ramadhani akisema hiki ni cha kutenda mema kama ilivyofanya TCB kwa kuandaa ibada hiyo ya Iftar.

"Lengo la mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kuhakikisha wanadamu tunazidi kumcha Mwenyezi Mungu kwa namna mbalimbali kama wenzetu walivyofanya leo kupitia Iftar hii," Shekhe Kawambwa alinena na kutilia mkazo umuhimu wa taasisi za fedha nchini kulihudumia taifa na kusaidia kujenga uchumi wa nchi.

Akizungumza katika Iftar hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Moshingi, aliwatakia Waislam nchini na duniani kote heri ya Mfungo Mtukufu wa Ramadhani akisema kuandaa futari kwao ni utaratibu na utamaduni wa miaka mingi.

"Huu umekuwa ni utaratibu wetu wa muda mrefu na ni utamaduni wa kitanzania na dunia nzima kwa ujumla. Kipindi cha funga ni wakati wa kutenda mema na kuwakarimu wenzetu," alisema huku akiishukuru BAKWATA na wadau wa benki hiyo kwa kujumuika na TCB kwenye hafla hiyo.

Alimshukuru Mufti Mkuu wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir Bin Ali, kwa kukubali kushiriki futari hiyo akisema hiyo ni heshima kubwa sana kwao.

Kuhusu TCB, Moshingi alisema taasisi hiyo ni miongoni mwa benki kongwe na zenye uzoefu mkubwa nchini kwa takribani miaka 100.

Aidha, alisema TCB haina mpinzani linapokuja suala la kuongoza kuwahudumia wananchi na taifa kwa ujumla.

# Spika ashauri madaktari bingwa wanaosomeshwa kurudi kazini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameishauri serikali kuweka masharti maalum yatakayowalazimisha madaktari bingwa wanaosomeshwa na serikali kurudi kwenye vituo vyao vya kazi wanapomaliza masomo.

Dk.Tulia alitoa kauli hiyo bungeni juzi baada ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kueleza namna serikali inavyokabiliana na uhaba wa madaktari bingwa kutokana na swali la nyongeza la Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, aliyehoji lini ahadi ya serikali iliyotolewa mwaka jana ya kupeleka madaktari bingwa 11 katika Hospitali ya Kitete itatekelezwa. Spika alisema madaktari hao wanaosomeshwa na serikali kupitia programu maalum wawekewe utaratibu maalumu utakaowataka kutoondoka katika vituo ambavyo walichukuliwa kabla ya kwenda kusoma.

"Serikali inatakiwa kuweka utaratibu mzuri kwa lengo la kuhakikisha madaktari bingwa hao wanarejea katika vituo vyao wakihitimu ili maeneo haya yasiendelee kuwa na uhaba," alisema.

Akitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo la madaktari, Waziri Ummy, alisema wizara hiyo ilipata kibali mwaka jana cha kuajiri madaktari bingwa, lakini hawakupatikana sokoni.

Alisema madaktari bingwa 400 wanasomeshwa nje na ndani ya nchi kwa njia ya seti unahusisha pia wahudumu katika fani hiyo wakiwamo manesi na wahudumu wa dawa za usingizi na pamoja na upasuaji kupitia programu inayoitwa Samia Suluhu Supper Specialists na kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilitengewa Shilingi bilioni nane.

Waziri Ummy alisema, wizara hiyo imeamua kutumia njia hiyo ya kuhamasisha madaktari waliopo katika hospitali mbalimbali ili wakasome udaktari bingwa kutokana na baadhi ya waliosomeshwa kutopatikana sokoni.

Pia, alisema wizara hiyo imefanya tathmini na kubaini baadhi ya hospitali zina madaktari bingwa na nyingine zina upungufu na kuamua kuwapanga upya kwa kuwatawanya katika hospitali zenye uhaba.

Awali, katika swali la msingi la mbunge huyo, alitaka kujua ni lini tatizo la ukosefu wa madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Kitete itatatuliwa. Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisema, Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Kitete hadi sasa ina jumla ya madaktari bingwa (5), daktari bingwa wa afya ya kina mama na uzazi (1), madaktari bingwa wa watoto watatu (3) na daktari bingwa wa upasuaji mmoja.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Askari wenye tabia hizi wazidi kushughulikiwa

**KWA** muda mrefu, kumekuwa na malalamiko dhidi ya baadhi ya askari wa polisi ambao wamekuwa wakikiuka maadili ya kazi zao. Vitendo hivyo vimesababisha kulipaka tope Jeshi la Polisi na kuonekana ndizo tabia za taasisi kwa ujumla.

Miongoni mwa vitendo ambavyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya askari hao ni kuwapiga wananchi na kuwasababishia wengine vifo na ulemavu wa kudumu, kuvujisha siri za watoa taarifa, kuomba na kupokea rushwa na kuwabambikia wananchi kesi zikiwamo za mauaji baada ya kukataa kutimiza haja za askari hao.

Kuwapo kwa vitendo vya aina hiyo na vingine, vilisababisha Rais Samia Suluhu Hassan kueleza kwa kinagaubaga mara kwa mara kuwa mambo hayo, yakiwamo ya mahabusu kufariki dunia kwenye vituo vya polisi, hayakubaliki katika utawala wake kwa kuwa vinaitia doa serikali yake. Aliwataka maofisa na askari wa jeshi hilo kubadilika na kufanya kazi zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu. Ili kuhakikisha jeshi hilo linarejea kwenye mstari wake, Rais Samia alifanya mabadiliko kwa kumteua Mkuu Mpya, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, kuchukua nafasi ya IGP Simon Sirro pamoja na kumteua Ramadhan Kingai kuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI). Kadhalika IGP Wambura amekuwa akifanya mabadiliko ya wakuu wa sehemu mbalimbali wakiwamo makamanda wa mikoa ili kuboresha ufanisi na matunda yake yameanza kuonekana.

Hata hivyo, Kama wahenga wasemavyo mazoea hujenga tabia, vitendo hivyo vimekuwa sawa na donda ndugu na jambo la kawaida kutokana na kukithiri na hata kuonekana ni sehemu ya majukumu ya askari hao. Yapo matukio ambayo yamekuwa yakiripotiwa siku hadi siku juu ya baadhi ya askari kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua hiyo imesababisha wananchi kukosa imani na jeshi hilo lililopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Hivi karibuni, kwa mfano, Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Morogoro wakiongozwa na aliyekuwa Mkuu wa Kikosi Wilayani Morogoro, Mratibu Msaidizi Aminiel Mosha, walirekodiwa katika video iliyosabazwa kwenye mitandao ya kijamii wakimshushia kipigo dereva wa gari dogo. Kitendo hicho kilishutumiwa na jamii wakiwamo wadau wa usafirishaji.

Kutokana na kitendo hicho, Jeshi la Polisi kupitia kwa kamanda wa Polisi wa Mkoa, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, lilitangaza kuwa askari hao tayari wameshaanza kuchukuliwa hatua za kinidhamu, ikiwamo kubadilishiwa majukumu. Sambamba na hatua dhidi ya askari hao, Kamanda Mkama ameagiza dereva aliyeshambuliwa na kupigwa aripoti kituo kikuu cha polisi cha mkoa ilia toe taarifa zaidi kama amepata madhara kiafya na kimwili.


Kwa ujumla, hatua iliyochukuliwa dhidi ya ofisa na askari hao ni ya kupongezwa kwa sababu kwa kiasi fulani, itapunguza tabia zilizokithiri za baadhi ya askari kujiona wako juu ya sheria kwa kuchukua hatua dhidi ya wananchi kinyume cha sheria. Huo ni mwanzo mzuri na ishara njema kwa jeshi hilo katika kuhakikisha haki inatendeka kwa wananchi wote.

Yako matukio mengi ambayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya askari ndani ya jeshi hilo ambayo yamesababisha kulichafua jeshi hilo, hivyo ni vyema hatua zikachukuliwa dhidi yao ili kukomesha ukiukwaji huo wa maadili. Mfano, mwaka jana kulikuwa na tukio la askari wa kituo cha Buguruni jijini Dar es Salaam kushiriki kupora nyama katika machinjio ya Vingunguti na kutokomea nazo, jambo ambalo lilileta fedheha kubwa kwa jeshi hilo.

Ni wakati mwafaka sasa, vitendo hivyo vinavyolishushia hadhi Jeshi la Polisi vikafika ukomo. Uongozi wa Jeshi la Polisi chini ya IGP Wambura kuchukua hatua kali dhidi ya askari ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili ndani ya jeshi hilo. Ni dhahiri kwamba hakuna lisilowezekana bali kinachotakiwa ni uthubutu katika kila jambo likiwamo la kusafisha taasisi kwa kuwachukulia hatua za kinidhanu wale wanaokiuka maadili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuporomoka maadili, enyi wazazi mko namba moja kuzibeba lawama

Na Adam Fungamwango

**KUMEKUWAPO** matamshi na makaripio mengi kwa siku za karibuni kuhusiana na mmomonyoko wa maadili kwa vijana, kuhusu uchafu huu unaohusu mapenzi au ndoa za jinsia moja.

Tumeona, hata viongozi wa ngazi mbalimbali za serikali, wakiwamo wabunge wanajitokeza kukemea suala hilo, ambalo limechukua nafasi kubwa kwa siku za karibuni.

Hata alipokuwa akifuturisha waumini mkoani Shinyanga, Mkuu wa Mkoa huo, Christine Mndeme, alisema maadili ya vijana kwa sasa yameshuka, ikiwamo kuiga mambo kutoka mataifa mengine na kuwaomba viongozi wa dini kulikemea suala hilo.

Katika futari hiyo iliyowashirikisha pia viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali mkoani humo, Mkuu wa Mkoa akatoa rai yake, akiwasisitiza viongozi wa dini mkoani humo na taifa kwa ujumla, kupambana na tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Nakubaliana kabisa na Mkuu wa Mkoa Mndeme, kwamba kwa miaka ya hivi karibuni kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili, ikiwamo vijana kutokuwa na heshima wala adabu na sasa limeenda mbali zaidi, kuja wimbi kubwa la uhusiano wa mapenzi ya jinsia moja.

Lakini, hayakuja hivi hivi, yana chanzo chake! Ni kiini kinachofaa kifutwe na kuondolewa kabisa. Kupungua maadili kulianza taratibu na kila mmoja nadhani alichukulia kama mzaha, lakini kwa sasa limekuwa tatizo kubwa sana.

Ni sawa kuna makaripio, kukemea na wengine wameenda mbali sana kutaka wanaume wakamatwe na wapimwe, kuonekana kama wana tabia hizo, lakini nadhani tulipiga hatua kutoka kelele na makaripio ya sasa, mpaka kibali kila mmoja achukue jukumu lake, ili kupunguza kitu kama hicho.

Kelele na makaripio ya sasa hayawezi kupunguza chochote, badala yake tuangalie tulipokosea. Binafsi naona kiini hasa cha mmomonyoko wa maadili kiko kwa wazazi na walezi, huku kwingine kukichangia asilimia ndogo.

Wapo wazazi hasa mijini hawako karibu na watoto zao, kutokana na 'ubize' na hata wanaporejea hawataki kujishughulisha kujua maendeleo ya watoto. Hii inawafanya watoto kulelewa na wengine, hasa 'wadada wa kazi', majirani, pia mitandao ya kijamii.

Kuna wazazi wenye uwezo, wamekuwa na tabia kuwadekeza kupita kiasi watoto wao. Hiyo inawafanya kutopitia changamoto zilizoko kwenye maisha yake yajayo, hasa watoto wa kiume.

Baba anashindwa kumpa koleo mtoto wake achimbe mtaro mdogo ili maji ya mvua yasituame, au kufyeka majani yaliyozonguka nyumba. Baadaye mtoto huyo atakuwa kijana asiyejua maisha magumu, hivyo anaangukia hatari ya mambo kama yanayolalamikiwa.

Wazazi au walezi, pia wajue ni hatari kumlaza chumba kimoja na mgeni yoyote, hata awe ndugu wa damu, kwa sababu asilimia kubwa ya wanaume wa aina hiyo 'wameharibiwa' tangu wadogo na ndugu wa karibu kama wajomba, baba wadogo na wakubwa, au rafiki.

Huku tunakopiga kelele na matokeo leo, ni matokeo ya madhara ya muda mrefu. Tuanze kupambana kuachana na tabia hizo, kupunguza mambo, pia viongozi wa dini au serikali zichukue nafasi zao.

Wazazi wengi tuko wavivu mno kulea, kiasi kwamba hata watoto wadogo wa shule ya msingi wanapelekwa bwenini. Huko ndiko umri wanakokutana na vitu vya ajabu.

Umri huo anatakiwa kulelewa nyumbani, kwa sababu ataanza kuiga tabia njema za baba na mama anaowaona na siyo wengine. Kuna tabia iliyozuka kwa wazazi kuwalipia watoto nauli ya mtu mzima kwenye daladala wakae, huku mtu mzima au mzee mwenye miaka 70 au 80 anabaki amesimama.

Hiyo nayo inawafundisha tabia mbaya watoto. Ni moja ya sababu zinazozaa mmomonyoko wa maadili, kijana wa miaka 20 kwa sasa hawezi kumpisha mtu mzima umri wa baba yake kwenye vyombo vya usafiri.

Nadhani katika hilo nalo, wazazi ndiyo wabebe lawama zaidi, kuliko wahusika. Kupunguza hayo yote, ni kubadilisha malezi, ili kukibadilisha kizazi.

Viongozi wa serikali na dini waje baadaye, lakini hili kwa kiasi kikubwa wazazi ndiyo wahusika wakuu na wanastahili lawama, pia wanawajibika kubadilika.

# Diaspora waanza kuwekeza nchini

**Na Faustine Feliciane**

WATANZANIA wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) wameanza kuitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuja kuwekaza nchini baada ya kuzinduliwa kampuni ya biashara za mtandaoni ya 'UzaSale'.

Kampuni hiyo iliyozinduliwa rasmi juzi, inamilikiwa na Watanzania watatu wanaoishi Minesotta nchini Marekani na itakuwa ikifanya kazi na kuweka makao makuu yake hapa nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mwanzilishi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Clement Marriot, alisema ujio wao kuwekeza nyumbani umetokana na mazingira mazuri ya biashara na ushawishi mkubwa wa serikali kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuja kuwekeza nyumbani.

"Ujio wa Rais wetu nchini Marekani na ushawishi wake umetufanya sisi Watanzania tunaoishi nje ya nchi kuanza kufikiria kuja kuwekeza nyumbani, kampuni hii itakuwa ikihusika na uuzaji bidhaa mbalimbali kwa njia ya mtandao, na sisi tutaendelea kuwashawishi watanzania wenzetu wanaoishi nje ya nchi na wana uwezo kuja kuwekeza nyumbani," alisema Marriott.

Alisema kampuni hiyo imelenga kutoa ajira kwa watanzania na kuwasaidia watu ambao hawana uwezo wa kukodisha maeneo ya biashara kwenye majengo makubwa na kuwapa nafasi ya kufanya biashara kupitia mtandao huo kwa gharama nafuu.

Alisema wapo watanzania wengi wenye uwezo wanaoishi Marekani ambao wana malengo ya kuja kuwekeza nyumbani, kuanzisha kampuni hiyo ya Uza Sale kutaongeza ushawishi kwa Diaspora kuja kuweka nyumbani.

Aidha, alisema kampuni hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na kampuni ya LK -Technology ya Marekani.

Kwa mujibu wa Marriott, Tanzania ni nchi mojawapo Afrika ambayo matumizi ya malipo kwa njia ya simu yanakua siku hadi siku kuliko Marekani ambako kampuni yake imefanya biashara kwa miaka zaidi ya 20.


# NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI ,KWA JINA LA SALUM JUMA NYANDOTO. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA KWA JINA LA SALUMU JUMA NYANDOTO 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI KWA JINA LA SALUM JUMA MARWA 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA KWA JINA LA SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 04/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | LILIAN FRANCIS MBETWA | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 100986,KIWANJA NAMBA 70 KITALU '18' | LEILA FRANCIS KAMA MLEZI WA AMIRI HAMISI IDDI | MAGOMENI | 5/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | GEOFREY FEDRICK MHAKILICHA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | SHAIBU SOZI SALUMU | MTUMBA-DODOMA | 08/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | VICTOR MOSES NNKO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | VICTOR MOSES NNKO | KIBAIGWA | 09/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | BENEDICTO WILSON MAGAYA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BENEDICTO WILSON MAGAYA | NZUGUNI | 08/05/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JOYCE STEVEN MSOFU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MONICA THADAYO CHISUMUNI | NG'HONG'HONA | 10/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | BIMLA ELECTRICAL SUPPLIES | VIWANJA (2) | RAJABU SIMEO MAJIGE | BUIGUIRI | 10/05/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | MAGRETH JOSEPH MASSAWE | NYUMBA | MAGRETH JOSEPH MASSAWE | NZUGUNI | 08/05/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | TITO KALAM SANGA | NYUMBA | TITO KALAM SANGA | KIBAIGWA | 09/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | OSCAR EMMANUELY MHEMBANO | NYUMBA | OSCAR EMMANUELY MHEMBANO | NTYUKA | 16/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | NYUMBA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | MPAMAA | 16/05/2023 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | ZEPHANIA MATHAYO MBATA | NYUMBA | ZEPHANIA MATHAYO MBATA | MSISI | 12/05/2023 SAA 03:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | INOCENCIA JANUARY LUBINGA | NYUMBA | PETRO JOSEPH MASADU | MSISI | 12/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JANVIER VOSTER LUBINGA | NYUMBA | JANVIER VOSTER LUBINGA | MSISI | 12/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | EDWARD WAMI KATEI | NYUMBA | EDWARD WAMI KATEI | MSISI | 12/05/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | HAPPYNESS MUSSA JEGU | KIWANJA | HAPPYNESS MUSSA JEGU | NZUGUNI | 08/05/2023 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | JOYCE SAMWELY ABRAHAM | KIWANJA | JOYCE SAMWELY ABRAHAM | NDACHI | 11/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JOSEPH TOBIAS MWAKYUSA | NYUMBA | JOSEPH TOBIAS MWAKYUSA | ZUZU | 11/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SHABANI SAID CHIBWANA | NYUMBA | SHABANI SAID CHIBWANA | VINGUNGUTI | 5/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ARIEL JOHN MNGEREJA | NYUMBA | ARIEL JOHN MNGEREJA | ZINGIZIWA CHANIKA | 09/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ZENA SOZI SALIM | NYUMBA | ZENA SOZI SALIM | KIMARA MAVURUNZA | 10/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | TAMIKA IZACK MWALUM | NYUMBA | TAMIKA IZACK MWALUM | KIBAGA KINYEREZI | 11/05/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMRANI SADIKI MGALULA | NYUMBA | AMRANI SADIKI MGALULA | CHANIKA | 09/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | VIWEGE MAJOHE | 12/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

MAJEMBE AUCTION MART KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA CHINI YA AKIBA COMMERCIAL BANK PLC Tutauza Gari ambayo ni mali ya Benki hiyo kwa njia ya Mnada.Taarifa za gari na tarehe ya Mnada huo kama inavyojieleza hapo chini

| JINA LA MMILIKI | NAMBA YA GARI | AINA YA GARI | MAHALI GARI ILIPO | MWAKA WA KUTENGENEZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| AKIBA COMMERCIAL BANK PLC | T 224 DBD | FORD RANGER | AKIBA BENKI TAWI LA MWANZA | 2014 | 5/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0754497396/0692836202**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217385702

# TANESCO kusambaza huduma vituoni

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limetangaza kufunga ofisi zake mbili jijini Dar es Salaam na wananchi watahudumiwa kutoka ofisi kuu pamoja na za viunga (vituo vya huduma).

Tangazo hilo la TANESCO lililotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano na Uhusiano, jijini Dar es Salaam juzi na kutaja ofisi zilizofungwa kuwa ni Tegeta pamoja na Viwandani.

"Kuanzia Mei Mosi, ofisi zetu za Viwandani na Tegeta zitafungwa rasmi...huduma zetu zitakuwa zikitolewa na viunga vilivyopo maeneo ya karibu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa TANESCO, wateja waliokuwa wanapata huduma Tegeta watahudumiwa na ofisi za Shirika hilo zilizopo Mbezi Beach pamoja na viunga vilivyopo Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Boko, Bahari Beach na Ununio. Viunga vingine kwa mujibu wa taarifa hiyo ni vilivyopo Mbeni JKT, Mbweni Mpiji, Kinondo, Mbopo, Bunju A, Bunju B na Mabwepande.

Kwa upande wa Viwandani, wateja hao watapata huduma katika ofisi ya TANESCO Tabata, Gongo la Mboto, Ilala pamoja na viunga vya Kiwalani, Vingunguti, Pugu, Buguruni, Karakata na NRRT.




Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Majadiliano ya Vijana ndani ya vyama vya Siasa 19, Rehema Omary, akizungumza wakati wa uzinduzi wa majukwaa ya majadiliano ya vyama vya Siasa, mkoani Dar es Salaam jana, ambao ni mradi wa kuimarisha Majadiliano ya vyama vya Siasa na kukuza ushiriki wa Vijana katika Siasa na uchaguzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Vijana 960 wafadhiliwa kupata mafunzo ufundi stadi

**Na Joseph Mwendapole**

Benki ya KCB kupitia taasisi yake ya KCB Foundation imeingia ubia na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) ili kuwawezesha vijana 960 nchini kupata mafunzo ya ufundi stadi ili kupunguza tatizo la ajira nchini.

Ubia huo wa asilimia 50 kwa 50 wenye thamani ya Euro 846,000 sawa na Sh. bilioni 2.2 ulianza Oktoba, 2021 hadi Mei 2023 utawawezesha vijana kupata mafunzo kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika sekta ya ujenzi ikiwamo fani ya umeme, uashi, ufundi rangi, ufundi bomba na uchomeleaji.

Mradi huo ulizinduliwa juzi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alipongeza juhudi zinazofanywa na benki ya KCB Tanzania na GIZ katika kufungua fursa kwa vijana nchini.

"Suala la uwezeshaji wa vijana ni muhimu sana katika kukuza uchumi. Hii inatokana na ukweli kwamba vijana ndio nguvu kazi ya Taifa hili; kundi hili ni kubwa, muhimu lenye umri wa kufanya kazi katika sekta mbalimbali.

"Niseme tu mmeonesha mnavyoguswa na masuala ya kukuza ajira kwa vijana wa kitanzania kwa kuwapa ujuzi na stadi za kazi kwa ajili ya kuwawezesha vijana wetu kujiajiri na kuajiriwa pia katika maeneo mengine. Nipende kuwapongeza KCB na GIZ kwa kuwawezesha vijana hawa na serikali tunaunga mkono jitihada hizi," alisema Waziri Mkuu.

Alisema serikali imeendelea kutekeleza programu mbalimbali zenye lengo la kuwawezesha vijana kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo KCB ili kuzalisha ajira milioni saba ifikapo mwaka 2025.

Mkurugenzi Mkuu wa KCB Group, Paul Russo, alisema benki ya KCB inatekeleza mikakati mbalimbali ambayo imelenga kuwezesha jamii kujikwamua na changamoto mbalimbali ili kuleta tija zaidi.

"Tunafarijika kuungana na wenzetu GIZ ili kuleta matokeo chanya na ya muda mrefu kwenye jamii na kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa nchi. Tunatambua umuhimu wa vijana katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na namna ambavyo sekta ya ujenzi inavyosaidia kuleta tija kwa watu wengi zaidi," alisema.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuchochea maendeleo ikiwamo kutoa fursa za ajira kwa watanzania hususani vijana.

Mkurugenzi Mkazi wa GIZ, Dk. Mike Falke, alisema: "Tunafarijika na ubora na matokeo ya ushirikiano huu ambao unaendana na mipango ya serikali katika kuongeza ujuzi na kuongeza ajira ikiwamo Mpango wa Kitaifa wa Kukuza Ujuzi na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano 2021/22-2025/26," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya KCB Bank Tanzania, John Ulanga, alisema dira ya benki hiyo ni kuleta mabadiliko kupitia vijana na makundi mengine hitaji ili kuleta athari chanya na za muda mrefu ikiwamo ujasirimali kwa kuwapa mafunzo ya usimamizi fedha, ujuzi wa mifumo pamoja na huduma kwa wateja ili biashara zao ziweze kukua zaidi.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa KCB Bank Tanzania, Cosmas Kimario, alisema benki hiyo itaendelea kutekeleza miradi ya kuwainua vijana ambapo kwa mwaka huu imejipanga kuwawezesha vijana wapya 5,000.

"Kwa KCB Bank mpango huu ni endelevu na kwa mwaka huu wa 2023 tumejipanga kuwawezesha vijana wapya 5,000 Tanzania bara na Zanzibar. Tunaamini hatua hii itafungua fursa kwa vijana wengi zaidi ambao wataweza kujiajiri na kuajiri vijana wengi zaidi hapa nchini," alisema Kimario.

# Mkono kuzikwa kwao Busegwe mwezi ujao

**Na Sabato Kasika**

MWILI wa aliyewahi kuwa Mbunge wa Musoma Vijijini na Butiama mkoani Mara, Nimrod Mkono, unatarajiwa kurejeshwa nchini mwezi ujao na kuzikwa kijijini kwao, Busegwe.

Mdogo wa marehemu, Zadock Mkono, alisema jana Dar es Salaam kuwa kikao cha ndugu kimeamua mwili usafirishwe kutoka Florida, Marekani ili akazikwe nyumbani kwao.

"Utaratibu wa kusafirisha mwili umeanza ukisimamiwa na binti yake na mke wake ambao wanasema utafikishwa nchini baada ya wiki mbili au tatu, hivyo ni wazi mazishi yatafanyika Mei," alisema Zadock.

Zadock alisema taratibu za kusafirisha mwili zinachukua muda mrefu na kwamba hata binti yake anataka kuja kumzika baba yake akiwa na watoto wake. Kwa mantiki hiyo, alisema inabidi awachukulie ruhusa shuleni na hata yeye apate ruhusa kazini ndipo waondoke.

"Kwa ratiba hiyo, ni wazi mazishi yatafanyika Mei lakini kabla ya hapo mwili utakaporejeshwa utafikishwa nyumbani kwake Masaki, Dar es Salaam. Heshima za mwisho zitatolewa katika Kanisa la Wasabato Magomeni kisha safari ya kwenda Butiama itaanza," alisema.

Zadock alisema mtoto wa marehemu anaomba wasamaria wema wamsaidie chochote walicho nacho afanikishe kusafirisha mwili wa baba yake kwa kuwa kuna wanafamilia 10 wanaotarajiwa kuja na mwili huo.

"Ukweli ni kwamba kwa idadi hiyo ya watu na mambo mengine, gharama ni kubwa, ndiyo maana anaomba msaada kwa Watanzania wenzake ili afanikishe safari hiyo ndani ya wiki mbili hadi tatu," alisema.

Kwa mujibu wa mdogo wake huyo, Mkono aliondoka nchini Julai, 2018 kwenda Marekani kwa ajili ya matibabu baada ya kuugua ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu (Alzheimer).

Mkono alikuwa Mbunge wa Musoma Vijijini kwa kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2015 na jimbo lilipogawanywa na kupatikana la Butiama, alililohudumia miaka michache akaenda kutibiwa.

Mwanasiasa huyo ambaye pia alikuwa mwanasheria maarufu, tangu alipoondoka kwenda Marekani, hakurudi nchini na jimbo la Butiama lilibaki wazi hadi uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mkono alizaliwa Busegwe Agosti 18, 1948 na kwa mujibu wa mmoja wa watoto wake, Abbas Mkono, ameacha mjane Mary Mkono na watoto watano.





## M/kiti CCM atoa siku 30 kupewa taarifa utengenezaji barabarara

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUMERU

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Noel Severe, ametoa siku 30 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi, kuwasilisha taarifa halisi ya mitambo ya halmashauri ya kutengeneza barabara ambayo kwa sasa baadhi yake haifanyi kazi.

Mitambo ambayo haifanyi kazi ni pamoja na katapila na mtambo wa kushindilia barabara, gari la kubebea mitambo ambalo lilipata ajali mkoani Kilimanjaro lilikopeleka mitambo na gharama ya matengenezo yake ni Sh. milioni 47.

Aidha, mwenyekiti huyo pamoja na wajumbe wa kamati ya siasa ya wilaya hiyo wamekerwa na kitendo cha watumishi wa Zahanati ya Bwawani, kulala kwenye wodi za wagonjwa huku ujenzi wa nyumba ya watumishi ya 'Two in One' ujenzi wake ukiwa unasuasua kwa zaidi ya miaka 13.

Akizungumza katika ziara hiyo jana, Severe alisema, haiwezekani mitambo ambayo imenunuliwa kwa fedha nyingi na inafanya kazi binafsi ambazo sio za halmashauri, huku wananchi wakikabiliwa na tatizo kubwa la miundombinu ya barabara kwa madai ya fedha za kutengeneza hakuna.

"Mkurugenzi ninakupa siku 30 ulete mbele ya Kamati ya Siasa ya wilaya, kuwa mitambo hiyo ilinunuliwa wapi kwa gharama ya shilingi ngapi, imeingiza shilingi ngapi na zimetumika kufanya kazi gani kwa sababu haiwezekani leo mnatuambia hapa kuwa mitambo ni mibovu imesimama mwaka mzima, inahitaji shilingi milioni 158 za kuitengeneza, wakati kwa siku mtambo mmoja ulikuwa unakodishwa kwa shilingi laki nane," alisema.

Alisema haiwezekani katapila ambayo ilikuwa haijafanya kazi mwaka mzima kutokana na ubovu, imenunuliwa magurudumu mapya mwishoni mwa mwaka juzi halafu yaliyopo kwa sasa ni kipara.

"Mmetuambia hapa kwamba katapila hii haijafanya kazi kwa mwaka mmoja sasa, kwa sababu ni mbovu, lakini pia mmetuambia kwamba mliinunulia magurudumu mapya mwezi Novemba 2021.

Swali la kujiuliza hapa imekuwaje magurudumu tunayoyaona kwenye katapila hili ni kipara wakati tangu magurudumu yanunuliwe haijawahi kufanya kazi," alihoji.

Kuhusu ujenzi wa nyumba ya watumishi katika zahanati ya Bwawani, Severe alimuagiza Msumi kutafuta fedha mara moja ili nyumba hiyo ikamilike.

"Nataka nyumba hii ikamilike sasa kwa sababu haiwezekani wananchi wametoa nguvu kazi pamoja na fedha zao kusaidia ujenzi huu, halafu bado halmashauri haitaki kulimalizia huku watumishi wakilala kwenye wodi za wagonjwa hasa wanawake wanaofika kwenye zahanati hii kwa ajili ya kujifungua.

"Ni hatari kwa watumishi kulala kwenye wodi za wagonjwa pamoja na samani zao, kwa sababu wanaweza kupata magonjwa ninaomba mkurugenzi tafuta fedha popote jengo hili likamilike, kwa sababu wananchi wameshatoa madirisha na vifaa vingine.

Claudia Muro, ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya wilaya, alisema watumumishi hao, bado ni wasichana wadogo wameonyesha uzalendo wa dhati kufanya kazi vijijini, lakini mazingira wanayoishi ni magumu kwa sababu wanaishi wodini.

# Miradi ya bil. 157/- kunufaisha hifadhi nne

**Na Tumaini Mafie**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameshuhudia utiaji saini wa miradi minane itakayojumuisha hifadhi nne za taifa yenye thamani ya Sh. bilioni 157.2.

Akizungumza juzi katika hafla iliyofanyika jijini Arusha, Mchengerwa alisema, wizara hiyo, haitaongeza muda bali watasimamia makubaliano yaliyo kwenye mkabata wa utekelezaji wa miradi hiyo, kati ya serikali na wakandarasi.

Kadhalika, alisema mtu yeyote atakayekwamisha utekelezaji wa miradi hiyo, atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi ya Tanzania. Alisema, kutokana na miradi hiyo kuchelewa kusainiwa na wako nyuma, aliagiza kazi ifanyike kwa haraka ili wizara hiyo iweze kupata nafasi ya kusaini miradi ya awamu ya pili. "Huu mradi wa Re grow unatakiwa ufanyike vizuri na haraka ili tuweze kupata mwingine awamu ya pili, kwa kuwa tumechelewa kuanza, ilitakiwa ianze tangu mwaka 2019, lakini hadi sasa mnaona tulipo," alisema Mchengerwa.

Pia, aliitaka wizara hiyo kuweka wazi mambo yote yanavyofanyika kwa kuwa fedha zinazotumika ni mali ya wananchi na wanapaswa kufahamu kinachoendelea.

Alisema endepo wananchi watapewa taarifa sahihi ya utekelezaji wa miradi hiyo, wataendelea kuwa na imani na serikali yao kwa kuwa fedha hizo ni mkopo wa Benki ya Dunia namna unavyofanyiwa kazi.

Mkurugenzi wa Hifadhi za Taifa, alitaja baadhi ya matatizo yanayoikabili hifadhi hizo, kuwa ni ubovu wa miundombinu, ujangili na alisema kupitia miradi hiyo, wanaamini itapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hilo.

"Tunaahidi kusimamia vyema miradi hii kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa kuwa tumejipanga kujenga viwanja sita katika hifadhi ambavyo vitagharimu Sh. bilioni 110," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas, alisema mtu yeyote atakayekwamisha miradi hiyo, ni vyema akaondolewa ili kupisha kasi ya ujenzi.



Mkurugenzi wa kampuni ya Franone Mining Ltd, Onesmo Mbise (kushoto), akipokea zawadi ya keki kutoka kwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Naisinyai, Mary Joseph wakati wa mahafali ya kwanza ya kidato cha sita shuleni hapo, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa shule hiyo, William Ombay. **PICHA: GIFT THADEY**

# Jamii kifugaji yatakiwa kuwapatia watoto urithi wa elimu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WANANCHI wa jamii ya kifugaji (Maasai), Kata ya Naisinyai, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuwapatia watoto wao urithi wa elimu ili kuwasaidia katika maisha yao kufikia malengo.

Alisema elimu ndio kitu muhimu kitakachowasaidia watoto kwa nyakati zijazo kufikia malengo badala ya kuwarithisha mifugo pekee.

Rai hiyo, ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd, Onesmo Mbise, wakati wa mahafali ya kwanza ya wanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Naisinyai, wilayani humo.

Mbise alisema pamoja na kuwa na mifugo, wafugaji wakiwapatia elimu watoto wao watakuwa na manufaa makubwa zaidi kwa kuwa wataweza kufanya mambo makubwa kupitia elimu.

Aliwapongeza wahitimu hao kwa kufanikiwa kupata elimu ya kidato cha sita na kuwataka wakati wakisubiri kufanya mitihani na kujiunga na vyuo mbalimbali waanze kuwatumikia Watanzania.

"Nawapongeza wanafunzi wote kwa kuhitimu kidato cha sita kwa kuwa miaka ijayo mtakuwa watu fulani muhimu kwenye jamii kupitia elimu mliyonayo hivi sasa," alisema Mbise.

Pia, aliwatakia heri wanafunzi wote 33 wafaulu mitihani yao ya kuhitimu kidato cha sita wanayotarajia kufanya mwanzo mwa mwezi Mei, mwaka huu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Naisinyai, William Ombay, alimshukuru mdau huyo wa elimu kwa kupitia kampuni yake kuahidi kukamilisha baadhi ya matatizo yanayowakabili.


"Tunashukuru kwa ahadi zako kuwa suala la ukosefu wa umeme kwenye bweni la wasichana umelibeba, pia visima vya kuhifadhi maji," alisema Mwalimu Ombay.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wa kidato cha sita, Joseph Emmanuel, alisema shule hiyo imeanzishwa mwaka 2006 ikiwa ya kidato cha kwanza hadi cha nne na mwaka 2021 ikapandishwa hadhi na kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

Emmanuel alisema wanafunzi 53 walipangiwa kuanza kidato cha tano, kati yao 40 wakaripoti, lakini walipungua na wengine saba kuhama na kubaki 33.

Diwani wa Kata ya Naisinyai, Taiko Laizer, alisema watampa ushirikiano wa kutosha mwekezaji huyo mzawa kupitia kampuni ya Franone Mining LTD inayochimba madini ya Tanzanite.

"Hii ni hatua nzuri ya mahusiano mema ya uwekezaji kupitia kampuni yako ya Franone Mining LTD na jamii ya kata ya Naisinyai, tunatarajia tutashirikiana vyema," alisema Taiko.





# Wawekezaji kupewa viwanja bure Biharamulo

**Na Daniel Limbe,**
BIHARAMULO

SERIKALI wilayani Biharamulo mkoani Kagera, imeahidi kutoa viwanja bure kwa wawekezaji wakubwa wenye maono ya kujenga wilaya hiyo kutokana na fursa za maeneo mengi ya uwekezaji.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa wilaya hiyo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, ACP Advera Bulimba, wakati akizungumza na wadau wa maendeleo wa wilaya hiyo katika hafla fupi ya kueleza mafanikio yaliyotekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani.

"Wilaya yetu imefanya mambo makubwa kwa kipindi hiki cha miaka miwili ya Rais Samia Suluhu ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa Sh. bilioni 56.9 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali na mikubwa ya maendeleo kwa jamii yetu," alisema ACP Bulimba.

Aliwakaribisha wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya wilaya hiyo na kuahidi kuwapatia viwanja bure watakaoleta miradi yenye kuchochea maendeleo ya wilaya hiyo kwa kufanya mazungumzo na mkurugenzi ili ampatie ardhi bila malipo.

Alitaja baadhi ya miradi iliyotekelezwa kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya barabara, ambayo awali ilikuwa kero kwa wananchi ikilinganishwa na sasa wananchi wanazitumia kwa kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko kuinua uchumi wa kaya na taifa.

Alitaja miradi mingine kuwa ni elimu ya msingi na sekondari, uboreshwaji wa huduma za afya, malipo kwa kaya maskini kupitia (Tasaf), huduma za majisafi na usafi wa mazingira, uongezwaji wa watumia umeme kupitia Shirika la Umeme Nchini (TANESCO).

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Biharamulo, Robert Malulu, alipongeza serikali kwa kuonesha nia ya kukuza maendeleo katika halmashauri hiyo na kwamba imesaidia kuinua ustawi wa jamii.

Mmoja wa wazee maarufu wa wilaya hiyo, Rwasa Kakuru, aliomba serikali kufanya jitihada kubwa za kusogeza huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria katika baadhi ya maeneo ndani ya wilaya hiyo.



Mjasiriamali, Evelyn John akiponda kokoto ili kujipatia ujira wa siku katika kijiji cha Mikwamba, kata ya Magila, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Bil. 4.6/- kuondoa kero ya maji Musoma

**Na Mathias Marwa,**
MUSOMA

SERIKALI imesaini mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 4.6 kwa ajili ya kumaliza kero ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi wa Mayani-Tegeruka-Kataryo katika mwendelezo wa mradi wa Mgango-Kiabakari-Butiama.

Akishuhudia utiaji wa saini wa mradi huo, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, alisema kuwa mradi huo utaanza na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji kwenye kata mbili za Tegeruka na Mugango zote zikiwa na vijiji sita katika Jimbo la Musoma vijijini, mkoani Mara na utakamilika ndani ya siku 180.

Alisema kwenye bomba la maji la Mugango-Kiabakari hadi Butiama lina uwezo wa kusafirisha na kusambaza lita milioni 35 kwa siku na Mamlaka ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira Musoma vijijini (RUWASA), ikiagizwa kuanza mara moja ili kuwapunguzia adha kina mama ambao ni waathirika wakubwa wa kero ya maji.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mayani, Kata ya Tegeruka walisema kuwa wakati wa kiangazi wanalazimika kuamka saa tisa usiku kuchota maji Mugango na hurudi nyumbani saa tatu asubuhi wakiwa wamechoka.

"Katika maeneo yetu bado tatizo la maji ni kubwa kutokana na kufuata maji umbali mrefu hali inayo sababisha wakati mwingi kuacha shughuli zetu za kila siku na mradi huu utatusaidia kumaliza adha hii," alisema Annamara Chacha, mkazi wa Tegeruka.

# Wasabato wafuturisha waislamu Shinyanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KANISA la Waadventista Wasabato Jimbo la Nyanza ukanda wa dhahabu (Nyanza Gold Belt Field) mkoani Shinyanga, limewafuturisha waumini wa dini ya Kiislamu mkoani humo, huku likikemea vitendo vya ushoga, ulawiti, ubakaji, na usagaji.

Askofu Mkuu wa jimbo hilo, Enoch Sando, akizungumza juzi wakati wa futari hiyo, alisema kanisa hilo linaamini kuimarisha mahusiano mazuri na viongozi wengine walio katika dini tofauti ili nchi iendelee kuwa na amani.

Alisema kuna vitendo viovu ambavyo vimeshamiri visivyo mpendeza Mwenyezi Mungu, vikiwamo vya ushoga, ulawiti, ubakaji na usagaji na kuwaomba viongozi wa dini ya kiislamu na madhehebu mengine waungane kuvikemea.

"Kanisa la Waadventista Wasabato tunawaomba viongozi wa dini ya kiislamu na madhehebu mengine, tuungane tuwe kitu kimoja kwa kulaani vitendo vichafu ambavyo vinaendelea hapa nchini vikiwamo vya ushoga, ulawiti, ubakaji na usagaji ili nchi yetu ibaki kuwa salama," alisema Askofu Sando.

Kanisa hilo pia lilikabidhi zawadi ya mbuzi, mchele kwa Shekhe wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Makusanya kwa ajili ya sherehe ya Eid, pia vitabu vya dini viitwavyo 'Jipatie Amani ya Moyo' ambavyo pia alipewa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi.

Shekhe Makusanya, alisema kitendo walichokifanya Wasabato cha kufuturisha kimedhihirisha kuwa binadamu ni ndugu wa damu moja na kina manufaa makubwa katika kutengeneza umoja, mshikamano, upendo na ushirikiano.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuombea nchi amani na kukemea vitendo vichafu yakiwamo matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambayo yanaichafua taswira ya mkoa huo.



Ukurasa 13

Kutapakaa machimbo Butiama kunavyoharibu mazingira



Ukurasa 12

LAMALYAMA GROUP

## Kinamama waathirika wa biashara wanyamapori, waliogeuka walinzi

HIMOFILIA

# Ugonjwa damu haigandi penye jeraha, anayeugua maradhi yake ya kudumu

**Na Christina Mwakangale**

KUNA ugonjwa uitwao himofilia. Wagonjwa wake ni wachache sana na hata ngumu kujitambua kuwa wanaugua, wengi hawajui. Ni asilimia tatu pekee ndio wanafahamu hali zao, ambazo huzaliwa nazo.

Kutobainika kunatajwa ni hatari, kwani inapotokea dharura ya kuhitaji upasuaji au ajali, mgonjwa huvuja damu kuliko kawaida, kutokana na taarifa za mhusika kutobainika. Mtu anapokosa chembe za protini zinazosaidia damu kuganda, baada ya mtu kujeruhiwa inakuwa shida kiafya.

Daktari Bingwa wa Damu, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Stella Rwezaura, ambaye ni Mratibu na Rais wa Chama cha Himofilia Tanzania, anasema hadi sasa, kuna wagonjwa, walezi na wataalamu 800 wa shida hiyo wamepatiwa elimu.

Anasema, ni elimu inayogusa kuugundua, kukabili, kutibu, pia tahadhari za kuchukuliwa kwa wanaougua, wengi wanaoumwa wakiwa watoto wanahitaji uangalizi. Anaendelea: "Bado kuna kazi kubwa ya kutoa elimu kwa jamii kwamba, watambue ugonjwa huu si wa kulogwa bali ni kama magonjwa mengine. Wanaougua hawajitokezi, wengi wanaishia kwenye tiba za kienyeji.

"Katika wagonjwa 6,300 tunaokadiria kuwapo nchini, kati ya Watanzania milioni 60, ni 200 tu tumewafikia na kuwatibu. Utaona tulivyo na safari ndefu kulifikia kundi hilo ambalo hatujui walipo, ndio maana tunatumia wadau tofauti kama vyombo vya habari, kuwafikia wagonjwa wengine," anasema bingwa huyo.



Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Jessie Mbwambo (kushoto) na Bingwa wa Magonjwa ya Damu MNH, Dk. Stella Rwezaura, wakimvisha zawadi ya kitenge Meneja Mkuu wa Shirika la Novo Nordisk Haemophilia, Denise Braendgaard, ambalo linaendesha mradi wa himofilia nchini. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Anafafanua sababu ni vinasaba vonavyoshika zaidi jinsia ya kike (X-chromosome) na asilimia 30 wanapata Himofilia bila ya kurithi, kutokana mabadiliko ya vinasaba.

"Mtu mwenye himofilia ataishi na ugonjwa huu maisha yake yote, hauponi. Tatizo hili hutibika inashauriwa kufanya uchunguzi ili kujua historia, afya, kubaini uwapo wa himofilia kabla ya kufanyiwa upasuaji na tohara," anasema.

**WANAOISHI NAYO**

Katika maadhimisho Siku ya Himofilia Duniani iliyoadhimishwa na MNH siku chache zilizopita, ilitanguliwa na mafunzo kwa wanahabari, wagonjwa, wazazi na walezi, shuhuda nazo zikitolewa na wagonjwa.

Edson Praygod (10), mwanafunzi wa darasa la tano, anasema wazazi wake walimwambia alianza kuugua tangu umri mwaka mmoja, hata akachelewa kufanyiwa tohara. Anaeleza: "Mwanzo nilishituka kwanza, nikawauliza maswali mengi baba na mama. Wakanijibu maswali yangu na wakanitia moyo na siku nilipofanyiwa 'circumcision' (tohara) walinitia moyo madaktari wakasema ninaweza.

"Nilipokuwa shuleni nilijisikia vibaya, wenzangu wote wamefanyiwa circumcision ila mimi tu. Nilikuwa siwezi kutoka nje, nilikuwa najihisi aibu sana. Nikawa naomba nikiamini ipo siku yangu na mimi sasa nimefanyiwa hivi, nipo jasiri, najisikia kuwa jasiri," anasema Edson na sasa anaeleza shukurani kwa waliomsaidia, akiwamo Dk. Rwezaura kwa kupigania hali yake kufika aliko sasa, akiendelea na tiba.

Dominic Seye, anayeugua ugonjwa huo, anasema tiba wanayoitumia inaitwa 'factor' kwa maana ya chembe zinazotumika kugandisha damu, akisema walipo mikoani, namna ya kuzitumia ni changamoto.

"Mimi naugua na tayari ninajitambua, wapo wasiojitambua. Wauguzi wengine hasa huko mikoani, zahanati au vituoni hawajui namna ya kuzitumia, tunapitia changamoto nyingi," anatamka na kufafanua:

"Hatupendi kuona mtoto aliye na himofilia leo, apitie tuliyopitia. Wataalamu wa afya, sindano zetu za kujichoma, tunazojichoma wengine hawajui kuzitumia ni ngeni kwao. Tuna imani watoto wetu hawatapitia haya."

James Kago, anayetokea nchini Kenya, anasema ameishi nao takribani miaka 40 sasa, tangu akiwa na mwaka mmoja. Hapo ana ufafanuzi: "Umoja wa Himofilia Kenya umesaidia kuwapo kwa ongezeko la kliniki kwa ajili ya huduma za ugonjwa huu. Tatizo kuu kwetu ni maumivu ya 'joint' (viungo) mara nyingi damu huvuja usiku kuanzia saa tano, hata kama

**INAENDELEA UK.14**

MAZINGIRA

LAMALYAMA GROUP

# Kinamama waathirika wa biashara wanyamapori, waliogeuka walinzi

**Na Jenifer Gilla,** aliyekuwa

BABATI

NI mwaka 2016, pale Lydia Joseph, mkazi wa Kijiji cha Ngoley katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati, hatousahau machungu aliyopitia yakileta mageuzi makubwa katika maisha na ukombozi dhidi ya biashara haramu ya wanyamapori kwa jamii yake.

Anasimulia mkasa uliomkuta mama huyo aliyekulia katika familia ya wawindaji, iliyopo mapitio ya wanyama ya Kwakuchinja, kwamba mnamo Aprili 6 mwaka huo, mwanawe akirithi mikoba ya uwindaji hata akamletea nyama ya punda ale, huku akienda kuuza nyama iliyosalia.

Lydia anasema, biashara ya uwindaji pasipo kibali maalum na kuuza nyamapori ilishapigwa marufuku na kulikuwa na doria kali dhidi yake. Haikupita hata saa moja, polisi walifika mlangoni mwake kumkamata, ila akafanikiwa kutoroka kwenda mjini Arusha kwa mtoto wake mwingine kujificha.

"Arusha nilikaa kama wiki mbili hivi, wakaja kunikamatia huko huko, nikarudishwa Babati nikapelekwa Magereza ambalo nilikaa miezi mine. Ikabidi watoto wauze baadhi ya mashamba yangu ili ipatikane faini ya shilingi milioni 2.5 ndio nikatoka. Huo ndio ukawa mwisho wa mimi kula nyamapori na mwanangu kufanya hiyo biashara," anasimulia Lydia.

Anawasimulia waandishi wa habari, kwamba Januari mwaka huu, akatoa takwimu za Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), John Noronha, katika mradi wa Tuhifadhi Maliasili, kwamba inakadiriwa kuna vifo vya wanayama 1069 vimetokea.

Pia inaangukia watu 642 waliojeruhiwa na kupata vilema vya kudumu kwa miaka saba, kutokana na migogoro kati ya wananchi na wanyama inayoendelea katika maeneo yanayounganisha hifadhi nchini (shoroba).

Anataja chanzo kikuu ni kufanyika kwa shughuli za kibinadamu katika maeneo wanayopita wanyama hao. Lingine ni uwindaji haramu, kinyume na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009.

Lydia ambaye sasa ni mhamasishaji wa uhifadhi wa wanyamapori, anasema baada ya kutoka jela aligundua kuwa si mhanga pekee wa biashara haramu ya wanyamapori, kwa kuwa asilimia kubwa ya wanawake walioenda kumpa pole, walimhadithia matatizo wanayopitia kutokana na biashara hiyo wanazoafanya waume zao.

## • Wakaa jela, kuuguza watoto, kudhuriwa...



Pundamilia wakivuka barabara katika shoroba ya Kwakuchinja, iliyoko Babati. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA**

> **Tayari Dola za Marekani milioni 37.5 sawa na Sh. bilioni 86.25, zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mapitio ya wanyama 'shoroba' ikiwamo kutoa elimu juu ya uhifadhi na kuwapa wanavijiji mitaji, ili kuachana na shughuli ya uwindaji haramu.**



Lydia Joseph; mdau wa kupigania usalama wa wanayamapori.

### MWENYEKITI KIKUNDI

Mwenyekiti wa kikundi Lamailama, Petronila Gobbi anasema kilichomvutia kuingia kikundi hicho cha uhamasishaji ni 'misukosuko' ya ulezi wa familia wanayopitia, baada ya mume wake kukamatwa na kukaa jela miezi sita, alipokamatwa akiuza nyama ya digidigi aliyeiwinda bila kibali.

Mume wake alimwacha na watoto wadogo watatu maisha yalikuwa magumu, kwa kuwa alimtegemea kuleta mahitaji nyumbani, hali iliyomfanya kuuza baadhi ya mali zake apate pesa za kulea watoto.

Anasema baada ya kuunda kikundi mwaka 2018, walitembelewa na taasisi ya kijamii ijulikanayo Community Support Initiative Tanzania (COSITA) kwa kushirikiana na Polisi wa Usalama Barabarani waliopata fedha kutoka USAID na kuwapa mafunzo ya umuhimu wa kuhifadhi wanyamapori kwa jamii yao na taifa kwa ujumla.

Petronila anasema walipatiwa fedha Sh. milioni nne kwa ajili ya kutumisha mfuko wao wa vikoba na kununua kuku 100 wa nyama, huku kila mwanachama akikopa pesa kwa ajili ya kuanzisha mradi wake binafsi.

"Maisha yangu yamebadilika. Hiki kikundi kimeboresha maisha yangu, kutoka kuwa mama wa nyumbani na sasa nina mifugo na biashara ndogo ndogo. Hata nilipomwambia mume wangu sasa biashara ya wanyamapori basi, alinielewa kwa sababu anaona naleta pesa ya kusaidia chakula wakati yeye akihamia kwenye kilimo" anasema.

### SIMULIZI ZA MADHARA

Mwanachama, Matilda Daniel, anasema alipata hekaheka ya kuuguza mtoto wake aliyevimba mdomo kuwa mwekundu, baada ya kula nyamapori ambayo hakuweza kuifahamu, ambayo ililetwa kwao imeshachunwa.

"Baada ya kupeleka mtoto hospitali nikaambiwa amekula kitu ambacho kimemdhuru, wakaniuliza alikuwa nyama gani? Nikashindwa kusema, kwa sababu hata mimi sikuijua. Kwa hiyo tatizo jingine ni kama hilo, tunaletewa nyama ambayo hata hatujui ni ipi matokeo yake inatudhuru," anasema.

Matilda anaeleza kuwa, tangu amejiunga na vikoba maisha yake yamebadilika, kwa kuwa kila mwaka anakopa pesa inayomsaidia kukuza ndoto yake ya kuwa mfugaji na sasa ana kuku takribani 30 waliotokana na pesa za mkopo.

Mkurugenzi wa USAID, John Noronha, anasema tayari Dola za Marekani milioni 37.5 sawa na Sh. bilioni 86.25, zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mapitio ya wanyama 'shoroba' ikiwamo kutoa elimu juu ya uhifadhi na kuwapa wanavijiji mitaji, ili kuachana na shughuli ya uwindaji haramu.

### SURA YA MAFANIKIO

Lydia Joseph, ambaye ni mhamasishaji mkuu wa kikundi hicho, anasema tangu wameanza kutoa elimu kwa jamii inayozunguka rasilimali hiyo, kadhia yenye madhara kwa wanyama imepungua kwa kiasia kikubwa.

Anaeleza kuwa elimu walioitoa imebadilisha mawazo ya jamii na kufikia hatua baadhi yao waanika njia mpya zinazotumiwa na wauzaji nyama hizo haramu, ikiwamo kutangaza kuwa wanauza mboga za majani, huku chini wakificha nyamapori.

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA



Mwonekano wa machimbo katika Mgodi wa Madini ya Dhahabu, Sirorisimba, uliopo wilaya ya Butiama mkoani Mara, ukionekana jinsi ulivyokatwa miti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kutapakaa machimbo Butiama kunavyoharibu mazingira

**Na Marco Maduhu,** aliyekuwa

BUTIAMA

SEKTA ya Madini inadumu chini ya usimamizi wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake 2017. Upande wa pili, kazi zao zimekuwa na athari ya mazingira kuondoa uoto wa asili, kutokana na ukataji miti hovyo, kwa ajili ya kupata magogo ya kwenye mashimo (maduara) ambayo hutumia kuingia chini ya ardhi kwa ajili ya kupasua miamba yenye madini.

Baadhi ya migodi iliyotembelewa na Nipashe iliyopo Halmashauri ya wilaya ya Butiama ni Mgodi wa Sirorisimba, Magunga, Nyamikoma kuona namna uoto wa asili, unavyoathrika kwenye maeneo hayo ya machimbo, kutokana na ukataji miti hovyo.

Hilo linachukua sura huku Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, inaongoza ili kuondoa uharibifu wa athari za mazingira katika Migodi, ni lazima sheria husika zizingatiwe. Pamoja na kuhakikisha kuwapo mipango, madhubuti itakayowapa wachimbaji wadogo hisa za kiuchumi, ili wawe na njia mbadala na kufanya uchimbaji kwa kuzingatia sheria za uhifadhi wa mazingira.

Ofisa Usimamizi wa Taka na Mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Karani Ruhumbika, anasema machimbo ya madini wilayani humo yameharibu mazingira, akinena: "Uoto wa asili ambao ulikuwapo kwenye milima ambayo inachimbwa madini haupo tena maeneo yamebaki kuwa jangwa,"

Anasema, wao kama serikali wamekuwa wakitoa elimu ya utunzaji mazingira, pamoja na kupanda miti ili kurudisha uoto wa asili kwenye milima inakochimbwa madini, lakini muitikio wake umekuwa mdogo.

Ruhumbika anasema, mipango ya serikali ni kuendelea kuhamasisha upandaji miti kwa kushirikiana na wadau, wakiwamo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ili kurudisha uoto wa asili uliopotea.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sirorisimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Butiama Ibrahim Mniko, anasema katika milima ya uchimbaji madini kwenye Mgodi wa Sirorisimba, uoto wa asili ulishapotea na wanachokifanya kwa sasa, wachimbaji ni kununua miti (mirunda) kwenye maeneo mengine na kuimarisha mashimo ya uchimbaji madini.

"Milima yote ambayo inachimbwa madini kwenye mgodi huu wa Sirorisimba, uoto wa asili ulishapotea miti yote ilishakatwa," anasema Mniko.

Msimamizi wa Machimbo ya Majengo yaliyopo kijiji cha Nyamikoma wilayani Butiama, Lucas Wasinyo, anasema wachimbaji wadogo wanachimba madini kienyeji, hivyo suala la ukataji miti ni lazima, kwa sababu ya kuiweka kwenye mashimo na hawana njia nyingine mbadala zaidi ya miti.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyamikoma, Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Godluck Makaja, anasema wachimbaji wanakata miti sana, lakini kuhusu suala upandaji miti, anasema ni ngumu kwao sababu wao ni watu wa kuhamahama, wakifuata mahali madini yapo.

Meneja wa Mgodi wa Irasanilo, uliopo Magunga wilayani Butiama Robert Lucas, anasema katika Mgodi huo matumizi ya miti siyo makubwa sababu baadhi ya miamba haitumii miti (Matimba).

Karani wa Mgodi wa Irasanilo, Mugare Kitoki, anasema maeneo yote nchini yanayofanya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, suala la uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti halikwepeki na kusema, kama kuna njia mbadala ya uchimbaji bila ukataji miti, wanaomba kupatiwa elimu hiyo.

**DED BUTIAMA**

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Revocatus Rutunda, anakiri machimbo madogo ya madini wilayani humo yameathiri mazingira, pamoja na kupoteza uoto wa asili kwenye milima inakochimbwa madini, miti ikiteketea.

Anasema Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, sasa kuna migodi mingi inayochipukia na wachimbaji hawana elimu ya kulinda mazingira, ndiyo sababu ya uharibifu wa mazingira na ukataji miti, umekuwa mkubwa hata kupoteza uhalisia wa uoto wa asili.

"Halmashauri tumekuwa tukijitahidi kupanda miche na kuisambaza ili ipandwe na kurudisha uoto wa asili na takwimu za mwaka jana tulipanda miti milioni 1.6, lakini suala la upandaji miti na ukuaji ni kitu kingine, tulipofuatilia miti hiyo baadhi tulikuta imelishwa na mifugo," anasema Rutunda.

Pia, anataja sasa wamepata wafadhili kutoka asasi ya Global Resource Alliance, wanaopanda miti katika milima miwili ya Kigoro na Mwikoro, ili kurudisha uoto wa asili, huku na wao kama serikali wakiendelea kuhamasisha upandaji miti, kupitia pia maadhimisho ya sikukuu ya mkoa, Mara Day, ya utunzaji mazingira kwa kupanda miti.

"Elimu bado inahitajika sana ya utunzaji wa mazingira na kuzuia mabadiliko ya tabianchi, kwa historia ya zamani katika wilaya hii ya Butiama, milima yote ilikuwa imefunikwa na miti, lakini baada ya kuanza shughuli za uchimbaji madini milima yote ipo wazi,"anaongeza Rutunda.

Anataja mikakati mingine ya serikali katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, ni kutunga Sheria ndogo kwa kila kijiji na akibainisha kuwa, tayari kuna vijiji viwili vya Kamgendi na Lyamisanga, ambavyo tayari wameshatunga sheria ndogo, mara baada ya kuona uharibifu wa mazingira unakuwa mkubwa.

**KUTOKA TFS**

Meneja Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Hafidh Saidi, anasema katika maeneo ya machimbo wilayani humo, miti mingi na uoto wa asili umeshapotea, kutokana na ukataji miti.

Anasema, TFS tayari wameshaanza programu kwa kushirikiana na serikali kupanda miti ili kurudisha uoto wa asili na mwezi Aprili, mwaka huu watafika kwenye maeneo yote ya machimbo wilayani Butiama, ili kutoa elimu kwa wachimbaji ya upandaji miti.

"Suala la upandaji miti ni jingine na kuikuza ni suala jingine, kabla ya kuanza kupanda miti kwenye maeneo ya machimbo, lazima tufike kwanza kutoa elimu kwa wachimbaji na baada ya hapo ndipo tupande ili itunzwe na kukua," anasema Said.

> **"Suala la upandaji miti ni jingine na kuikuza ni suala jingine, kabla ya kuanza kupanda miti kwenye maeneo ya machimbo, lazima tufike kwanza kutoa elimu kwa wachimbaji na baada ya hapo ndipo tupande ili itunzwe na kukua.**

**OFISA MIRADI**

Ofisa Miradi kutoka Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Clay Mwaifani, anasema tatizo lipo kwenye maeneo mengi ya machimbo, madogo juu ya uharibifu wa mazingira ni ukosefu wa sheria ndogo ngazi ya vijijini.

Anasema kuwapo sheria hizo ndogo kutakuwapo na uwajibishaji hasa kwa watu ambao wanaharibu mazingira, pia muitiko wa upandaji miti utakuwa mkubwa sababu ya adhabu.

Mwaifani anasema pia sheria zipo zinasema 'kata mti panda mti'na kutoa ushauri katika maeneo ya machimbo, sheria hiyo inapaswa iongezewe makali kidogo, ukikata mti mmoja panda miti 30 ndiyo italeta tija na kuzuia uharibifu wa mazingira.

# Ugonjwa damu haigandi penye jeraha, anayeugua maradhi yake ya kudumu




Mjumuiko wa wagonjwa na madaktari wao, katika maadhimisho ya Siku ya Himofilia, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**INATOKA UK.11**

uligongwa (jeruhiwa) mchana."

Anaendelea: "Tunawapigia madaktari wetu kuanzia usiku, hapo ndio muuguzi unahitajika. Mara nyingi nilimwambia kuanzia saa sita usiku ndio 'bleeding' labda puani, inaanza usiku. Kuna kinadada zetu wakati wa mwezi, anakwenda siku zaidi ya tisa hadi 10 hawajitambui, sasa kuna suluhisho waje."

### WANAOLEA WATOTO

Regina Valence, anajitambulisha kuwa mzazi wa watoto wawili wanaougua himofilia, pia ni Mwenyekiti wa Wanawake Wanachama wa Chama cha Himofilia Tanzania, akisema

kwenye vikao vyao hujadili shida ya malezi, uchumi duni na watoto wao kupewa adhabu ya viboko shuleni, majeraha yanapotokea huwa chanzo mtihani wa damu kumtoka mtoto.

"Unapolea watoto hawa ni changamoto wanavimba magoti, ukuaji ni duni, akianguka tatizo. Kubwa zaidi ni kutengwa na jamii, kuna wakati familia inakutenga, wanaona kila mara wanakuhudumia.

"Familia zetu ushirikiano ni duni, unakuta mwanaume anakaa pembeni. Kwenye chama chetu unakuta na kinabibi ambao wanalea wajukuu, kwa sababu wazazi wao wanaona wanatumia muda mwingi kuwahudumia watoto, wanashindwa kufanya kazi. Anaona bora ampe mama yake mtoto alee.

"Watoto wa kike tulio nao kwenye chama kwenye mzunguko wao wa kila mwezi, wanaenda siku zao nyingi hadi wanalazwa. Wanashindwa kuhudhuria masomo na kurudi nyuma," anaeleza mwanamama huyo, akiongeza kuna wakati ni adimu kliniki na utunzaji wake unahitaji eneo baridi hasa katika friji, huku adhabu ya viboko kwa watoto wao shuleni inawahuzunisha zaidi.

"Watoto wetu wanaosoma kwenye shule za umma, changamoto wanachapwa, viboko, damu inavilia kwenye mwili wake. Tunaomba mradi uwezeshe watoto wetu wapate kliniki, na tufadhiliwe masomo ya ujasiriamali, wengi uchumi ni duni, kinamama tuinuke kiuchumi," anasema Regina.

### DALILI NA UTAMBUZI

Daktari wa Magonjwa ya Damu kutoka MNH, Gurishaeli Walter, anasema kuna aina mbili za himofilia; A na B na wengi wanaugua A, amabayo ni asilimia 80 ya wagonjwa wote. Hapo, sababu kuu ni mtu anakosa vichocheo vya damu kuganda, akitoa ufafanuzi himofilia huathiri jinsia ya kiume.

Anawaelezea: "Wagonjwa wengi hawajitokezi huamini kulogwa. Wengine waliolazwa wanadai watoto wao wametupiwa kitu. Dalili ya ugonjwa ni viwiko kuvimba, magoti, damu huvuja hasa kwenye maungio."

Hapo anatoa ushauri wawe wanapumzika kuwekewa barafu maeneo ya viungo au kwenye sehemu inakoanza uvujaji damu kama vile puani, ili kupooza mishipa ya damu kuendelea kutanuka.

Anasema mwanamke ndiye mbebaji wa vinasaba vya himofilia na kwamba utambuzi wa ugonjwa ni kufanyiwa vipimo hususan watoto wadogo tangu kuzaliwa na Dk. Gurishaeli anatahadharisha jamii kuepuka vyanzo vinavyochangia kuvuja damu, pia wadhibiti uvujaji pale inapotokea.

"Watu wanaougua himofilia hawapaswi kuwa wanamichezo. Iwapo akivuja damu ndani ya ngozi ni hatari na hatari kubwa ikivuja katika ubongo, anaweza kupata kiharusi. Ikitokea jeraha, unaweza kumuweka barafu ili misuli isinyae, apumzike na 'factor' itumike kuinua kiwango cha damu kutovuja," anaeleza Dk. Gurishaeli.

### TIBA MAZOEZI

Mtaalamu wa mazoezi viungo kutoka hospitalini Muhimbili (physiotherapist), Abdallah Makalla, anakiri wagonjwa hufika kwenye mazoezi mepesi kliniki, wakishauriwa hata kwenye tendo la ndoa wasitumie nguvu sana, kwani ni tendo lenye msukumo mkubwa wa damu, hasa kwa mwanaume.

Mratibu wa kuongeza Upatikanaji Huduma ya Magonjwa ya Damu, ikiwamo Himofilia nchini, Dk. Rwezaura na Mratibu Mwenza wa Kenya, Dk. Kibet Shikuku,ndoa wanasimamia uratibu huo, unaofadhiliwa na asasi ya kimataifa, Novo Nordisk Fonden (Novo Nordisk Haemophilia Foundation)

Dk. Rwezaura anasema kupitia mradi huo kuanzia mwaka 2020, wameshatoa mafunzo kwa wataalamu wakiwamo wauguzi na madaktari 555, wazazi na walezi 200 na wataalamu wa mazoezi viungo, takribani 30

"Wagonjwa wengi hufika kwenye kliniki damu zinavuja na kliniki ya MNH hatuna siku ya mapumziko, kwa sababu muda wowote huja wagonjwa wa aina hii," anasema.

Dk. Shikuku anasema, mabadiliko yanawezekana hasa kwa kutumia vyombo vya habari, ili kuongeza takwimu za wanaougua ugonjwa huo.

### HATUA ZA SERIKALI

Katika kuadhimisha siku ya ugonjwa huo, MNH ilizinduliwa maabara yenye mashine za kisasa na uwezo wa kupima sampuli za himofilia 180 kwa saa, mgeni rasmi akiwa Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, anasema magonjwa ya damu awali yalikuwa hayagunduliki mapema kutokana na mengi, ikiwamo uhaba wa vifaa.

Anasema, maabara hiyo itaongeza upatikanaji huduma za magonjwa ya damu, ikiwamo himofilia na selimundu, kusaidia utambuzi mapema kwa wanaougua.

"Sasa wataalamu wamepewa mafunzo pamoja na madaktari, wauguzi, wafiziotherapia, ili kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa hawa," anasema Prof. Nagu.

Wito wake kwa MNH ni kuendelea kujengewa uwezo hospitali za kanda, rufani na mikoa, ili huduma zipatikane huko, badala ya kuzifuata Muhimbili pekee.

# Kinamama waathirika wa biashara wanyamapori, waliogeuka walinzi

**INATOKA UK.12**

Chifu wa kitongoji wa Eluway, Leteiva Loburu, anasema moja ya mambo yanayochangia kushamiri uwindaji haramu katika eneo hilo, ni imani potofu iliyoenea kuwa baadhi ya nyama kama vile punda inaponeshaa magonjwa ikiwamo kifua, miguu na kusafisha figo.

"Sasa unakuta kundi linaoingia katika mtego huo ni wanawake, kwa sababu ni watu wa kuamini vitu kwa haraka. Wao wakiambiwa tu 'hii ni dawa ya kitu fulani' na ukiangalia ndani ana mgonjwa atakuwa ananunua kila siku," anasimulia kiongozi huyo.

Sasa anashukuru elimu iliyotolewa na misaada ya kimaendeleo waliopewa na mashirika mbalimbali, ikiwamo Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (JUHIBU), imepunguza migogoro kati ya wanyama na binadamu, sasa wanaweza kukaa eneo moja bila ya kuleteana madhara.

Katibu wa JUHIBU, Benson Mwaise, anasema wanashirikiana na wadau wengine wa uhifadhi, ikiwamo TAWA (Tanzania Wildlife Management Authority) na USAID kuhakikisha wanamaliza tatizo uwindaji haramu katika eneo la Kwakuchinja kwa manufaa ya wanakijiji na wanyama.

Anasema, baadhi ya mikakati yake ni kutoa elimu za uhifadhi kwa wanakijiji na kutoa gawio linalotokana na shughuli za utalii katika Hifadhi ya Wanyamapori ya Tarangire kila mwaka kwa wanakijiji, wanayoitumia kwenye miradi ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa shule pamoja na kutunisha mifuko ya vikundi cha kinamama ya vikoba.

"Kupitia njia hizi jamii imeelewa imeona umuhimu wa kuhifadhi maliasili hii muhimu kwa utalii nchini, sasa hivi na wenyewe wanashiriki kutunza, hata wakiona swala amepotea au ameumia watatoa taarifa au kumleta hapa ofisini, kwa kweli tunashukuru wadau ikiwamo USAID wanaotuunga mkono mafanikio ni makubwa," anasema.

# Barabara ya njia nne itakavyokuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dodoma, amesema mradi wa wa ujenzi wa barabara ya lami ya njia nne ya mzunguko ndani ya Jiji la Dodoma itakayokuwa na urefu wa kilometa 112.3, utakuza uchumi wa wakazi wa mkoa huo na nchi.

Leonard Chimagu aliyasema hayo juzi alipotoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa waandishi wa habari.

Alisema, mradi huo umegawanywa katika awamu za utekelezaji na makandarasi wawili tofauti.

"Ukikamilika utapunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dodoma na magari makubwa ambayo yanakwenda nje ya Dodoma hayatapita mjini, yatapita katika barabara hiyo huku ajira zaidi ya 1,000 zikizalishwa kupitia mradi huo," aliafanua.

Chimagu alisema kipande cha kwanza kitahusisha ujenzi wa kuanzia Nala-Veyula-Barabara ya Arusha-Mtumba-Ihumwa (bandari kavu) ikiwa na urefu wa Kilometa 52.3 na Mkandarasi wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)na kugharamu Sh. bilioni 100.84.

Alisema, ujenzi wa kipande cha pili cha barabara hiyo unaanzia Ihumwa (bandari kavu)-Matumbulu-Nala itakayokuwa na urefu wa kilometa 60 ambao Mkandarasi wa Kampuni ya AVIC International na kugharimu Sh. bilioni 120.86.

Pia, alizungumzia miradi mingine inayojumuisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami wilayani Mpwapwa (kilometa 50).

Chimagu alisema kuwa, ndani ya mkoa huo kuna mradi unasanifiwa ambao utahusisha ujenzi wa barabara za lami katikati ya jiji (Km 43).

Mhandisi wa Miradi kutoka TANROADS Mkoa wa Dodoma, Colman Gaston alisema kipande cha pili cha barabara hiyo ya mzunguko kutoka Ihumwa (bandari kavu) hadi Nala, utekelezaji wake umefikia asilimia 18.4.

Mhandisi Mshauri wa mradi huo kutoka kampuni za Inter Consultant and Pace na CTC Crown Tech, Issa Mjema alisema watasimamia kazi hiyo na kuhakikisha inakamilika kwa wakati (Machi 2025).

# Waziri: Tulifanya kosa kubwa kufuta mabalozi wa nyumba 10

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro amekiri serikali ilifanya kosa kufuta mfumo wa mabalozi wa nyumba 10, akiutaja ni uamuzi uliosababisha mmomonyoko wa maadili unaoshuhudiwa sasa nchini.

Dk. Ndumbaro alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa alipofungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Kosa kubwa tulilolifanya ni kufuta mabalozi wa nyumba 10, tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi, tukaona kuwa hawa ni watu wa CCM (Chama Cha Mapinduzi) na kuachana nao, lakini ukweli ni kwamba wale walikuwa na umuhimu mkubwa sana katika jamii zetu.

"(Mabalozi) walikuwa wanamfahamu kila mtu katika eneo lao na kujua tabia za kila mtu, hata kama mgeni akihamia eneo lingine, tabia zake wanazijua, lakini sasa tulipuuza na kuacha kutumia mabalozi wa nyumba 10, hali ambayo inatugharimu hivi sasa," Dk. Ndumbaro alisema.

Waziri huyo alisema tayari wizara yake imeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Bunge kufanya utafiti ili kubaini sababu zinazochangia kuongezeka kwa matukio ya mmomonyoko wa maadili nchini.

"Hivi sasa kumekuwapo malalamiko mengi katika jamii juu ya ongezeko kubwa na mmomonyoko wa maadili na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson hivi karibuni aliniagiza kufanya utafiti ili kubaini nini shida katika hali hii ya kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili," alifafanua.

Dk. Ndumbaro alisema tayari ameshaunda timu ya kufanya utafiti huo na kuja na mapendekezo ambayo yatasaidia kukabilina na ongezeko la makosa ya maadili nchini.

"Lakini pia hivi sasa hakuna sheria ambayo itatungwa ama kufanyiwa marekebisho kama haijafanyiwa utafiti wa kisheria na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Awali waziri huyo aliwataka viongozi wa baraza hilo kutimiza wajibu wao na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia katiba ya nchi, sheria, taratibu, miongozo, mila na desturi za kitanzania.

"Baraza la Wafanyakazi lisiwe sehemu ya kuhamasisha mambo ambayo hayana maslahi kwa taifa letu, lazima mfanye mambo yenu kwa kutetea maslahi ya watumishi mkizingatia katiba ya nchi, sheria, taratibu, weledi na miongozo mbalimbali," aliagiza Dk. Ndumbaro.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi alisema lengo la kikao hicho ni kujadili utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya mwaka 2023/24.

"Kikao hiki pia kitatumika kuendelea kuhimiza watumishi kufanya tathimini ya utendaji wao wa kazi ambao tumekuwa tukiufanya kila wiki," alisema.

Alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 ofisi yake imefanikiwa kuajiri watumishi 50. Kati yao, 48 ni mawakili wa serikali na wawili wataalamu wa TEHAMA.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara ya lami ya njia nne ya mzunguko jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 15/- kupunguza kero ya uhaba wa maji Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida umepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 15.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi 37 ya maji katika mwaka wa fedha wa 2023/24 ili kupunguza kero ya maji mkoani hapa.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Singida, Lucas Said alibainisha hayo jana alipoelezea mikakati yao, kipaumbele kikitolewa kwa taasisi za elimu na afya kupatiwa huduma ya maji kila unapojengwa mradi wa maji.

Alisema miradi hiyo itakayojengwa katika mwaka huo wa fedha, itaongeza upatikanaji wa maji vijijini mkoani hapa kwa asilimia 10 kutoka asilimia 68 hadi asilimia 78.

"Hadi kufikia Juni 2025 kwa mikakati ambayo RUWASA tumejiwekea, kiwango cha upatikanaji wa maji kitafikia asilimia 86 ambayo ni zaidi ya lengo la asilimia 85 lililowekwa kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)," alisema.

Said alisema wakati wa kujenga miradi ya maji, RUWASA imekuwa ikihakikisha kila taasisi zilizopo eneo husika kama shule za msingi na sekondari, vyuo, zahanati, vituo vya afya na hospitali zinapatiwa huduma ya maji kwa sababu maeneo hayo yanakuwa ni ya kimkakati.

Alisema kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 unaoisha Juni mwaka huu, zaidi ya Sh. bilioni 11 zilipokewa mkoani Singida kutoka Mfuko wa Taifa wa Maji na Mfuko wa Malipo kwa Matokeo kwa ajili ya kujenga miradi mbalimbali ya maji ambayo mingi imekamilika na mingine ipo hatua za mwisho za ujenzi.

"Ipo miradi inayotekelezwa kwenye wilaya tano za Mkoa wa Singida ambayo lengo kubwa ni kuhakikisha tunafikia asilimia 85 ya upatikanaji wa maji kama ilivyoainishwa kwenye ilani ya CCM ifikapo mwaka 2025 (ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 hadi 2025)," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji Mkoa Singida Vijijini ni asilimia 64 na ifikapo Juni mwaka huu, kiwango kitaongezeka na kufikia asilimia 68 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miradi ambayo fedha zake zipo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/23.

"RUWASA ilipoanza Julai 2019, hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Singida ilikuwa ni asilimia 49.5 lakini hadi kufikia Machi mwaka huu, imefikia asilimia 64, hivyo tuna uhakika wa kufikia malengo ya asilimia 85 kutokana na serikali kutupatia mtambo (mashine) wa kuchimbia visima," alisema.

Said alisema mtambo huo ulipokewa mkoani Singida Februari mwaka huu na sasa umeshatumika kuchimba visima sita Singida Vijijini, vinne wilayani Ikungi na sasa upo katika Wilaya ya Manyoni ambako vimechimbwa visima vitano, akisisitiza kila Wilaya kutachimbwa visima.



# Halmashauri, TFS waungana kudhibiti ukataji wa miti

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wameharibu matanuri 10 ya miti iliyokuwa imeandaliwa na baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Kambikatoto, Kata ya Sangambi wilayani humo kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde aliongoza operesheni hiyo jana akiwa amefuatana na baadhi ya viongozi wa wilaya, maofisa wa TFS na askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo).

Alisema uamuzi huo ni utekelezaji wa makubaliano ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambao walikubaliana kuanza operesheni ya kuwakamata wananchi wanaobainika kuchoma moto misitu na kukata miti.

Alisema hatua hiyo ni jitihada za kuinusuru Wilaya ya Chunya dhidi ya uharibifu wa mazingira ambao umechangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo kwenye vyanzo vya maji, ufugaji na ukataji miti.

Ripoti ya mwaka jana ya TFS, ilitaja wilaya hiyo kuongoza kitaifa kwa ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

"Tunaendelea na operesheni ya kuwakamata wale wote wanaohusika na uharibifu wa mazingira, ninaamini hatua hii itasaidia sana kuokoa uoto wa asili ambao ulipotea kutokana na shughuli za kibinadamu, na operesheni ya uchomaji matanuri haya ni jitihada zetu," alisema Mwanginde.

Aliwataka wananchi kuacha mara moja shughuli za uchomaji wa mkaa wilayani humo bila kuwa na kibali kutoka kwenye mamlaka zinazohusika na usimamizi wa mazingira.

Pia aliwataka viongozi wa wilaya kushirikiana kuhakikisha wanasimamia operesheni hiyo ili kuokoa ikolojia na uoto wa asili ambao kwa kiasi kikubwa umeharibiwa na wananchi ambao ni watumiaji wa nishati ya kuni na mkaa.

Katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon aliwahimiza viongozi wa vijiji na vitongoji kusimamia sheria ndogo za kuwaadhibu wananchi wanaobainika kuharibu mazingira.

Aliwataka viongozi hao bila kujali uhusiano wao kwenye jamii, kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria hizo wanaoharibu mazingira kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kujenga hofu na kuachana na tabia ya kukata miti ovyo.



Ofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Innocent Lupembe akiteketeza kwa moto tanuri 10 za miti wilayani humo jana, mali ya wananchi wa kitongoji cha Kambikatoto, kata ya Sangambi ambazo zilikamatwa na uongozi wa halmashauri ya wilaya hiyo zikiandaliwa kuchoma mkaa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Ulaji wa 'fedha mbichi' waundiwa mkakati kuukabili

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) umeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo cha Ufundi Arusha kutengeneza dira za maji ili kuepuka matumizi ya fedha mbichi zinazokusanywa na vyombo vya watumiaji maji vijijini.

Kaimu Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya, Erast Saronga alibainisha mkakati huo alipofungua mafunzo ya mpango biashara kwa vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii kutoka mikoa ya Songwe na Mbeya.

Alisema hatua hiyo inalenga kuepukana na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambaye katika taarifa yake ya mwaka 2021/22 amesema RUWASA ilibainika kukusanya fedha bila mashine za POS na hivyo kuikosesha serikali mapato.

"Jukumu la RUWASA ni kuvijengea uwezo vyombo vya watumiaji maji ngazi ya jamii ili vijiendeshe vyenyewe kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019 na kwamba mafunzo hayo yatasaidia fedha kukusanywa ndani ya mfumo ili kudhibiti upotevu wa mapato," alisema Saronga.

Aliongeza kuwa vyombo 55 vya watumiaji maji kutoka mikoa ya Songwe na Mbeya vimeshiriki mafunzo hayo yakiwahusika wenyeviti na wahasibu katika kila chombo kufundishwa namna usimamizi wa miradi ya maji, uendelevu wa huduma za maji vijijini.

Barnabas Tuligunga, Kaimu Meneja Uendeshaji na Matengeneza wa RUWASA, alisema mafunzo hayo yanalenga kuleta mabadiliko ya usimamizi wa vyombo vya watumiaji maji pamoja na upangaji wa bei zitakazozingatia utalaamu wa kisayansi.

Aliosema wanawafundisha washiriki kuzingatia ubora wa maji kwa kuhakikisha wanafuatilia huduma za upatikanaji wa maji na kupima kwenye maabara kila baada ya miezi mitatu, kwa mujibu wa sheria.

"Mpaka sasa tumeshatoa mafunzo kwa mikoa saba, tulianza na Tabora, Lindi, Mtwara, Rukwa, Kilimanjaro na sasa tupo Mbeya.

Lengo letu ni kufikia mikoa yote nchini ili kuwasaidia wasimamizi hawa kujifunza namna ya usimamizi wa mikataba kwa wateja wao, uandaaji wa bajeti na matumizi ya kielekroniki katika ukusanyaji wa fedha," alisema.

Aliongeza kuwa katika kuboresha huduma za utoaji maji, RUWASA itafunga dira 125 nchi nzima kwa kuanzia ili kupima ufanisi wake na kwamba malengo ni kuyafikia maeneo yote baada ya kujiridisha na utendaji kazi wake.

Nuhu Nyambulapi, Mratibu wa Vyombo vya Watumiaji Maji wilayani Chunya, alisema tayari wamepokea dira za maji kwenye Kata ya Kiwanja na kinachosubiriwa ni kuona namna zinatavyofanya kazi.

Aliishuruku RUWASA kwa kuja na utaratibu huo, akiutaja utasaidia kupata gharama halisi za matumizi ya maji na fedha ambazo zitakuwa zinalipiwa benki ili kujiepusha na mianya ya rushwa.

# DC, Spika kusaidia watoto wanaoishi mazingira magumu

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa kwa kushirikiana na Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson wamepanga kununua mahitaji ya watoto yatima na wanaoishi mazingira magumu 200 ikiwa ni sehemu ya kusherehekea nao sikukuu ya Eid el Fitr.

Malisa alibainisha hayo juzi wakati wa hafla ya kufuturisha waumini wa dini ya Kiislamu iliyoandaliwa na Taasisi ya Tulia Trust ambapo zaidi ya wakazi 1,000 wa Jiji la Mbeya walishiriki.

"Tuna kila sababu ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Spika wa Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson katika kuwahudumia wananchi wake.

"Dk. Tulia ametusaidia kuwakwamua wananchi kiuchumi kupitia mikopo mbalimbali inayotolewa ikiwamo ya vyombo vya moto, bajaj na bodaboda pamoja na mitaji kwa wajasiriamali ambao kupitia Taasisi ya Tulia Trust wamefanikiwa kukuza mitaji yao na kupiga hatua," alisema.

Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalambaha alisema wanaendelea na dua za kumwombea Spika Tulia ili apate maisha marefu kwa kuwa amekuwa na mchango mkubwa kuwaletea maendeleo.

Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya, Dourmohamed Issa alisema ni wakati sasa waumini wa dini ya Kiislamu kuungana na kushirikiana na serikali katika kuliombea Taifa kupiga vita vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Sabasaba, Ally Mbika alisema jamii ikiwa mstari wa mbele kuwafichua watu wanaojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia, itaisaidia serikali kuchukua hatua dhidi ya wanaohusika.



# Watendaji sekta umma watakiwa kuongeza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wa sekta za umma wametakiwa kuongeza ushirikiano katika taasisi zenye uhusiano na mambo ya Muungano na zisizo za Muungano ikiwa ni sehemu ya kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwataka kushirikiana kuwatumikia wananchi wote.

Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema hayo wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Haroun Ali Suleiman mjini Unguja.

Alisema zipo wizara ambazo sio za Muungano, lakini zina uhusiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwamo masuala ya kimataifa na mikataba yake.

Aidha, alisema Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano utekelezaji wa majukumu yake unakwenda sambamba na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mengi.

Alisema, yapo mambo yanayohusu utawala bora na ripoti zake za kimataifa, nchi zote mbili hutakiwa kufanya matayarisho ya ripoti zake kwa pamoja.

"Hizi ni wizara mbili ambazo sio za Muungano, lakini zimekuwa na uhusiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake kuwatumikia wananchi wa pande zote mbili," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Haroun Ali Suleiman alisema, ushirikiano wa wizara hizo ni muhimu katika kuleta ufanisi wa majukumu ya watendaji pamoja na kuwasaidia wananchi kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili.

Alisema, wizara hizo mbili zinashughulikia masuala ya watumishi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano ikiwamo Tume ya Ajira za Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano inayoshughulikia ajira katika taasisi za Muungano.

Alisema, Wizara hiyo inashirikiana na taasisi binafsi za serikali ya jamhuri ya muungano zinazosaidia masuala ya msaada wa kisheria kwa wananchi mbalimbali ikiwemo wasiokuwa na uwezo kuona wanapata haki kwa mujibu wa sheria.

Naye Mwenyekiti wa chama cha makatibu mahsusi wa Tanzania Bara, Zuhura Maganga, alisema wanakusudia kufanya mkutano Zanzibar ambao utahudhuriwa na wajumbe 6,000 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara.



Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi (wa tano kulia), akikabidhi baadhi ya vifaa vya kusaidia kupumua kwa watoto wachanga na mitungi 52 ya oksijeni na vifaa vyake kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume kwa ajili ya vituo vya afya 14 vya Serikali, mkoani humo jana. Kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la nchini Ujerumani GIZ, hospitali ya CCBRT sasa ina uwezo wa kutengeneza oksijeni na kubakiza ziada kwa ajili ya vituo vingine ili kusaidia wagonjwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Samia ahimiza kudumisha amani, utulivu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewataka wananchi kuendelea kudumisha amani na utulivu ili kutoa fursa kwa serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo na kukuza uchumi.

Dk. Samia alisema hayo juzi katika salamu zilizotolewa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, wakati alipomwakilisha katika futari kwa wananchi wa mikoa miwili ya Pemba.

Alisema serikali zote mbili zinafanya kazi kubwa ya kuleta maendeleo ya kisiwa cha Pemba ili kufanana na sehemu nyingine hatua ambayo itasaidia na kuleta mabadiliko makubwa.

Alisema, njia pekee ya mafanikio yote hayo ni kuimarika kwa amani na utulivu hatua ambayo itatoa nafasi kwa serikali kutekeleza miradi yake muhimu ya maendeleo.

"Serikali zenu mbili zimejipanga kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo kwa wananchi wa Pemba ambapo huu ni wakati wa kudumisha amani na utulivu," alisema.

Aidha, aliitaka jamii kuzingatia maadili ya mila silka na utamaduni wa wananchi wa Zanzibar ambao umerithiwa kutoka kwa wazazi wao.

Aliwataka wazazi kusimamia maadili hayo na kufuatilia nyendo za watoto wao kuona hakuna matukio yanayokwenda kinyume na utamaduni wa Watanzania.

"Nawaomba wazazi kufuatilia nyenzo za watoto wao kuona kwamba wanaishi kulingana na maadili, mila na utamaduni wa Watanzania," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahoro Masoud, alipongeza juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali mbili za kukifungua kisiwa cha Pemba katika miradi ya sekta ya uwekezaji na miundombinu.

Aliitaja miradi hiyo ikiwamo ujenzi wa barabara ya Chake Chake hadi Wete yenye urefu wa kilomita 22 ambayo inakwenda kuiunganisha mikoa miwili katika miundombinu ya barabara.

Aidha, alisema ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba ni hatua kubwa muhimu ambayo sasa inakwenda kukifungua kisiwa hicho katika sekta mbalimbali ikiwamo mawasiliano na utalii.

# Kampuni yaagizwa kukamilisha ujenzi tangi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Mawasiliano, Ardhi, Nishati ya Baraza la Wawakilishi, imeiagiza kampuni ya Simba Developer Limited, iliyokabidhiwa ujenzi wa tangi la maji katika kijiji cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, kukamilisha ujenzi huo kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa makubaliano yao.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yahya Rashid Abdallah, aliyasema hayo jana alipofika katika kijiji hicho kukagua mradi huo ambao umeanza mwaka jana na maendeleo yake yanaenda vizuri licha ya kuwapo kwa changamoto.

Alisema mradi huo unategemewa kumalizika Machi, mwaka huu na kwa sasa umefikia asilimia 78 licha ya changamoto ya ucheleweshaji wa vifaa.

Alisema, serikali imeamua kwa makusudi kupeleka mradi huo kwa lengo la kuondoa kiu na changamoto inayowakabili wananchi wa Tumbatu hasa katika masuala ya huduma ya majisafi na salama.

Hata hivyo, aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa kuendelea kushirikiana na serikali na wameridhishwa na uwapo wa mradi huo na kuonesha utayari kuona maendeleo hayo yanawafikia kwa wakati.

Katibu wa Kamati ya maji ndani ya Kijiji cha Tumbatu, Hassan Mwadini Haji, alisema wanashirikishwa, lakini changamoto iliyopo ni jiografia ya kisiwa hicho kuzungukwa na bahari.

Naye, Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaban Ali Othman, alisema, wizara itahakikisha inaimarisha ushirikiano mzuri na kamati ya maji ndani ya kijiji hicho ikiwamo kuondoa vikwazo vilivyokuwapo.

Alisema lengo ni kupata maji, hivyo wizara itahakikisha wanafanya kazi kwa ushirikiano ili lengo la serikali lifanikiwe na wananchi wa kijiji hicho kutumia huduma ya maji safi na salama kama walivyokuwa wananchi wingine.

Mhandisi mshauri wa kampuni hiyo, Adam Peter, aliahidi kukamilika ujenzi huo kama walivyokubaliana juni mwaka huu ambapo awali walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya kufika kwa vifaa.

Ujenzi wa tangi la maji katika kisiwa cha Tumbatu ni miongoni mwa matangi 10 yanayojengwa kutokana na fedha za ahuweni za UVIKO-19 na litachukua lita za maji milioni moja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**NEEMA KITALANGWA SOLWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S.0249/2010 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LORETO GIRLS SEKONDARI mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NY/RB/485515/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED HUSSEIN OMARY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI CANTER yenye usajili namba T253 BQM, CHASSIS NAMBA: TY2FE659H6DN00529 na ENGINE NAMBA: Y2FE659H6DN. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/135948/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAWADI ALEX SANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T 555 CFB. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MKB/RB/1459/2023**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATED) OF MANYONI AT MANYONI**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3/2023**

**In the Matter of the Estate of the Late NASSON NTABALIZO**

**And**

**In the Matter of Application for Grant for Letters of Administration**

**By**

**NAHOL NASSON NTABALIZO.............PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grand for letters of Probate and administration in made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 21st day of April, 2023 of the publication of this citation in the News Paper.

Dated at Manyoni this 5th day of April, 2023.

S.J. KAYINGA
RESIDENT MAGISTRATE
MANYONI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSACK AZARIA SHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SCANIA yenye usajili namba T 533 BVS , CHASSIS NAMBA: 044326622 na ENGINE NAMBA: 00WX8865. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/137182/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**THERESIA DEUS MUGASSA,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye NO **CSI20072446,** INDEX NO **S1071-0202** kilichotolewa na BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA kupitia shule ya Secondary St Mathew Mwaka 2012 Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/136621/2023**

**CHE LUZINGA LAW ATTORNEYS**
**Advocate, Notary public and Commissioner for Oaths**

**Ref: Che / ridhiwani / 03/ 2023**
**17th April,2023**
**Kwa:**
**Abdurahman Mbwana,**
**Mwanahawa Mbwana,**
**Rehema Mbwana Twalib,**
**Mama Mamsap Baliy,**
**S.L.P. 178,**
**Mwarongo- Tanga.**
**YAH: TAARIFA YA WITO WA KIKAO CHA FAMILIA TOKA KWA RIDHIWANI MBWANA**

**Kichwa cha habari hapo juu chahusika.**
Ofisi yetu inamuwakilisha RIDHIWANI MBWANA ( Mteja wetu kwenye shauri la Mirathi Namba 43 la 1979 ambapo Bwana RIDHIWANI MBWANA ni msimamizi wa Mirathi ambapo katika hatua za kutekeleza usimamizi wa Mirathi hiyo Mteja Wetu anapaswa kugawa nyumba ya marehemu. Hata hivyo, kwa nia njema ya Mteja We tuanakusudia kupata mawazo ya warithi wa marehemu ili kuamua njia njema ya kumalizia ugawaji wa mirathi ya marehemu. Kwa barua hii tunapenda kuwaandikia na kuwataarifu wewe ABDURAHMAN MBWANA, MWANAHAWA MBWANA, REHEMA MBWANA TWALIB na MAMA MAMSAP BALIY, kwaniaba ya Mteja wetu, kuwa unaombwa kufanya kikao cha familia na Mteja Wetu kwa siku na muda ambao mtakubaliana.

Kwa kuongezea, tunaomba kukutaarifu kuwa ikiwa hamtaweza kukaa pamoja na familia yenu yaani Mteja wetu na ndugu wengine, Mteja wetu atachukua maamuzi ya kuuza mali zote za marehemu na kugawa pesa kwa warithi wote na hakutakuwa na taarifa nyingine Ahsante.

**Yona Lucas (Wakili)**
**Kwaniaba ya: Che Luzinga Law Attorneys**
**Nakala Kwa:**
- **Ridhiwani Mbwana Twalibu**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA GEITA**
**MAOMBI NA 12/2023**
**MTAKOBA LWAKAYEYE.......MLETA MAOMBI**
**VERSUS**
**MWENGE LUTEMA**
**HELENA KAZIMOTO**
**RHODA KAZIMOTO........WAJIBU MAOMBI**

Kwa **RHODA KAZIMOTO** popote alipo unafahamishwa kwamba mwombaji tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhisi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba wilaya Geita, maombi haya yamepangwa tarehe 24/4/2023 kwaajili ya kutaja/kusikilizwa katika ofisi za Baraza saa 3 Asubuhi.

Hivyo basi unaamriwa kufika shaurini wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote aliyeruhusiwa kisheria. Nakala za madai zinapatikana katika ofisi za Baraza.

**KAA UKIJUA** kwamba kushindwa kufika kwako, baraza litasikiliza shauri na kutoa hukumu/maamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya baraza hili leo tarehe 30/3/2023

**E.MASAO**
**MWENYEKITI**
**30/3/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

MEDARD MODEST MSHASHA anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye namba za usajili T 916 AFT, T 836 ARU na T 586 ALG zilizotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb No. DAR/URA/RB/126874/2023.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO....08.............of 2023**

**IN THE MATTAER OF THE ESTATE OF THE LATE DEMETRIA HOKELAI SHEMWETA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**

**BY AGNES HOKELAI SHEMWETA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of May 2023
Dated at Korogwe this 18 day of April 2023


# OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## India kuipiku China idadi ya watu

**NEW YORK,** Marekani

UMOJA wa Mataifa umesema ripoti imeonyesha kuwa ifikapo katikati ya mwaka huu, India itakuwa nchi ya kwanza kwa idadi ya watu duniani.

Katika ripoti hiyo imeeleza China itapitwa na india kwa idadi ya watu milioni tatu

Ripoti ya hali ya dunia ya Fuko la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya idadi ya watu, (UNFPA) ilisema India itakuwa na watu bilioni 1, 426,800,000, huku idadi ya watu wa China ikiwa 1, 425, 700,000.

Takwimu rasmi zinabainisha kuwa idadi ya watu wa China ilipungua mwaka jana, hiyo ikiwa mara ya kwanza kwa miongo sita.

Mbali na India na China, ripoti hiyo ya UNFPA imekadiria kuwa na idadi ya jumla ya watu dunia itafikia 8,045, 000,000 ifikapo katikati ya mwaka huu. **DW**

## Moto waua wagonjwa 29

**BEIJING,** China

Watu 12 wamezuiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano baada ya moto kuteketeza hospitali moja mjini Beijing na kusababisha 29, kufariki dunia.

Moto huo, ni miongoni mwa matukio mabaya zaidi kutokea katika miaka ya hivi karibuni, ulizuka katika Hospitali ya Changfeng majira ya saa 7:00 usiku.

Ndugu wa watu walioathirika walipandwa na hasira baada ya kufika hospitalini hapo saa chache bila kupewa taarifa zozote,

"Saa saba au nane zimepita na sikupokea hata simu," jamaa mmoja aliambia China Youth Daily.

Wengi walisema walitumia usiku kucha wakijaribu kuwatafuta wapendwa wao.

Wale ambao waliokolewa walihamishiwa katika hospitali nyingine kwa matibabu.

Wakizungumza katika mkutano na wanahabari siku ya Jumatano, maafisa walisema uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa cheche za moto zilizotolewa wakati wa kazi za ukarabati zililisababisha kulipua rangi iliyohifadhiwa kwenye eneo la mkasa .

Miongoni mwa waliozuiliwa ni mkurugenzi na naibu mkurugenzi wa hospitali hiyo, pamoja na mkuu wa kampuni inayosimamia kazi za ukarabati.

Picha kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha wagonjwa wakiruka kutoka madirishani kukimbia huku moshi mzito ukitoka nje ya jengo hilo. **BBC**



Wanawake na watoto wakisubiri huduma ya matibabu nje ya kituo cha afya ya msingi katika kijiji cha Belwa, wilayani Kishanganj nchini China.**PICHA: REUTERS**

# Hali bado ngumu Sudan, hospitali 16 zalipuliwa

**KHARTOUM,** Sudan

MAPIGANO makali yanaendelea kwa siku ya tano nchini Sudan, baadhi ya maeneo nyeti ikiwamo hospitali zikilengwa katika mashambulizi.

Tangu kuanza kwa mapigano hayo Jumamosi iliyopita, pande zote mbili,vikosi vya jeshi la nchi hiyo na wanamgambo wa kikosi maalum (SRF) wanaendelea kupambana katika mitaa ya mji wa Khartoum na miji mingine ya jirani.

Mwandishi wa BBC aliyeko mji mkuu wa Khartoum, Mohamed Osman alisema mapigano yanaendelea katika baadhi ya maeneo ya mji huo yakiwemo makao makuu ya jeshi.

Ukubwa wa mapigano hayo hayajafahamika, lakini wakazi wa mji huo walisema bado wanasikia milio ya risasi.

Majenerali wawili hasimu, ambao wanajeshi wao wamekuwa wakipigania udhibiti, walikuwa wamekubali kusitishwa kwa mapigano ili kuruhusu misaada ya kibinadamu na raia kuondoka katika maeneo kwamba ili kupata misaada ya matibabu, lakini hilo halikutimia.

Mkuu wa misaada wa Umoja wa Mataifa, Martin Griffiths, alisema wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu wanashambuliwa na kunyanyaswa kingono.

Alisema, ofisi ya Umoja wa Mataifa huko Darfur Kusini imeporwa.

**Ninaweza kukuambia kwa uhakika kabisa, kwa usahihi kabisa, na unaweza kuingiza maneno yangu katika itifaki yoyote kwa taasisi yoyote katika ngazi za juu hadi leo, hakuna mpiganaji hata mmoja wa kijeshi nchini Sudan.**

Wakati huo huo, mkuu wa kundi la mamluki la Wagner la Russia, Yevgeny Prigozhin, alisema kuwa kampuni hiyo ya kijeshi ya kibinafsi haijawai kuwepo nchini Sudan kwa zaidi ya miaka miwili.

"Ninaweza kukuambia kwa uhakika kabisa, kwa usahihi kabisa, na unaweza kuingiza maneno yangu katika itifaki yoyote kwa taasisi yoyote katika ngazi za juu hadi leo, hakuna mpiganaji hata mmoja wa kijeshi nchini Sudan," alisema katika chapisho kwenye mtandao wa Kepka Prigozhina, wa Telegraph.

Alikuwa akimjibu mwandishi wa habari wa jarida la lugha ya Kifaransa la Jeune Afrique, ambaye aliuliza kama Wagner Group inaunga mkono kundi la wanamgambo wa Sudan la Rapid Support Forces (RSF) katika mapigano yanayoendelea na wanajeshi.

Katika hali ya kutisha, muungano wa madaktari wa Sudan ulisema kuwa hospitali 39 hazina huduma kati ya 59 katika mji mkuu, Khartoum na majimbo ya jirani baada ya kushambuliwa.

Kamati kuu ya madaktari wa Sudan (CCSD) ilisema katika taarifa yake kwenye Facebook kuwa hospitali 20 pekee ndizo zinazofanya kazi kikamilifu au kwa kiasi.

"Kati ya hospitali ambazo zimeacha kufanya kazi, kuna hospitali tisa ambazo zililipuliwa na hospitali 16 ambazo zililazimika kuhamishwa," CCSD ilisema.

Mapigano yanaendelea katika mji wa Khartoum na maeneo mengine ya Sudan huku jeshi na jeshi la wanamgambo wakilaumu kukiuka mapatano ya kibinadamu ya saa 24 ambayo yalikuwa yaanze kutekelezwa Jumanne jioni.

Kwa upande mwingine, serikali ya Tanzania imesema, raia wake wapatao 210 waliopo nchini Sudan, kati ya hao, 171 ni wanafunzi wapo salama.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo Stergomena Tax.

Waziri Tax, alisema Tanzania inasikitishwa na hali ya kuzorota kwa amani nchini Sudan kufuatia mapigano yanayoendelea kati ya jeshi na wapiganaji wa kikosi cha RSF.

"Serikali imeendelea kufanya mawasilano ya mara kwa mara na ubalozi wetu uliopo mjini Khartoum, ili kujua hali inayoendelea. Tunao Watanzania takriban 210 nchini Sudan, 171 ni wanafunzi, na wengine ni maafisa wa ubalozi na raia wengine. Hadi sasa hakuna Mtanzania aliyeripotiwa kuathiriwa na mapigano hayo. Namshukuru balozi wetu kwa kuhakikisha usalama wa raia wetu nchini humo," alisema wziri Tax. **BBC**

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA YAFURAHIA MAFANIKIO YAKE 2022/23

Na Mwandishi Wetu

UONGOZI wa JKT Tanzania FC umeweka wazi kwa sasa tayari malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Championship msimu huu na kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao yametimia kwa asilimia 90.

JKT Tanzania inayonolewa na Kocha Mkuu, Malale Hamsini, ndio vinara wa Ligi ya Championship wakiwa na pointi 62 huku nafasi ya pili ikishikwa na Pamba ya Mwanza yenye pointi 51, kila timu imebakiza mechi tatu ili kumalizika kwa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa JKT Tanzania, Kapteni Speratus Lubinga, alisema timu yao imejipanga kufanya vyema kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika michezo mitatu iliyobaki na kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara kwa heshima.

**Lubinga alisema anafahamu kufanya vyema kwa timu yao kulitokana na uongozi wa kikosi cha JKT kuwa bega kwa bega na benchi la ufundi la timu hiyo na kuwahamasisha wachezaji wakati wote wanapokuwa ndani na nje ya uwanja.**

"Sina mengi lakini natoa shukrani za dhati kwa uongozi mzima wa Jeshi la Kujenga Taifa likiwa chini ya Mkuu wa JKT Meja Jenerali, Rajabu Mabele, pamoja na Mkuu wa Tawi la Utawala, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, ambao wamekuwa wakiongeza hamasa kwa wachezaji ya kupata matokeo mazuri," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza mpaka sasa wametimiza asilimia 90 ya malengo yao kuelekea kukata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao.

Alitaja mechi tatu walizobakisha ni dhidi ya Kitayosce ya Tabora, Pamba, ambazo watacheza ugenini na watamaliza msimu nyumbani kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kwa kuwakaribisha Mashujaa.

"Kikosi kipo imara, lengo letu ni kuhakikisha tunaibuka na ushindi na kutwaa ubingwa wa Ligi ya Championship kwa msimu huu, tutakuwa tumetimiza maagizo ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa ambaye alitaka kuona kikosi kinarejea Ligi Kuu katika msimu ujao, sina shaka na wachezaji wangu, wanajituma kwa kuhakikisha timu inarudi," aliongeza.

Ametoa wito kwa wadau na mashabiki wa JKT kujitokeza kwa wingi ili kuongeza hamasa kwa wachezaji katika mechi zilizobakia.



Mshambuliaji wa Bilo FC ya jijini Mwanza (kulia), akipambana kumtoka nyota wa JKM Park Queens katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Soka ya Wanawake Daraja la Kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jana asubuhi. Bilo walipata ushindi wa mabao 3-2. **PICHA: TFF**

# *Mbagala Queens, Allan Queens, kicheko*

Na Saada Akida

KATIKA kuhakikisha wanaendeleza soka la wanawake nchini, Kampuni ya Mchezo wa Kubashiri ya Meridianbet imetoa zawadi ya vifaa mbalimbali vya michezo kwa timu za Mbagala Queens ya Dar es Salaam na Allan Queens kutoka jijini, Dodoma, imeelezwa.

Mbagala Queens inayoshiriki Ligi ya Mkoa wa Dar es Salaam (U-20) wakati Allan Queens yenyewe inashiriki Ligi Daraja la Kwanza ya Wanawake inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet, Martina Nkurlu, alisema kampuni yao inaamini vifaa walivyotoa zikiwamo jezi zitawasaidia katika michezo yao na hatimaye kufikia malengo ya klabu.

Nkurlu alisema, wanafahamu soka la wanawake linafanya vizuri na kuwasaidia kuwapa morali ya kupambana katika mashindano wanayoshiriki.

"Huu ni mwanzo tu, tumeona tuanze na timu hizi mbili (Mbagala Queens na Allan Queens), kwa sababu hawa walitufuata siku chache zilizopita na kutupa barua rasmi kuomba sapoti yetu, tunafahamu wanajiandaa na mashindano ya Ligi ya Daraja la Kwanza, tukaona tuwatafute na kuwaongezea nguvu," alisema Nkurlu.

Aliongeza wanatarajia kuendelea kusaidia timu nyingine ili kwenda na sera ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwekeza katika michezo hasa soka la wanawake.

## Kitayosce yaahidi kuisimamisha JKT

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Kitayosce FC, Henry Mkama, amesema hawatakubali kuwa 'mgongo' wa JKT Tanzania katika mbio za kupanda daraja watakapoikaribisha katika mechi ya Ligi ya Championship itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Mkama aliliambia Nipashe wanaendelea vyema na maandalizi kwa ajili ya kuzisaka pointi tatu na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za kupanda daraja kama ambavyo wapinzani wao wanatamani.

"Wachezaji wako tayari, wamechangamka na mechi wanaitaka, mashabiki wameamka wamekuwa wakihudhuria kwa wingi mazoezini kuwapa moyo na kuwatia nguvu kwa sababu wanataka kuiona Ligi Kuu msimu ujao. Tumebakisha mechi nne, tunahitaji pointi tisa ili tukamilisha mipango yetu," alisema kocha huyo.

Kimahesabu, JKT Tanzania inayoongoza ligi hiyo kwa pointi 62, inahitaji pointi mbili tu ili kufikisha pointi 64 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile katika ligi hiyo.

Kitayosce inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 50 na ikikabiliana na upinzani mkali kutoka kwa Pamba inayokamata nafasi ya pili ikiwa na pointi 51.

## Shikangwa, Simba Queens Ligi Kuu hawakamatiki

Na Adam Fungamwango

WAKATI |Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema siri ya kuendelea kufanya vyema katika Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania ni uwapo kwa kikosi kipana, mshambuliaji wake, Jentrix Shikangwa, ameendelea kuzitikisa vyavu za wapinzani.

Baada ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mkwawa Queens, Lukula alisema uamuzi wa kumpa kila mchezaji nafasi ya kucheza kunasaidia kuwapa mapumziko nyota wengine na kurejesha viwango vyao wanaporudi dimbani.

"Kila mtu anapata nafasi ya kucheza, wengine wanapumzika hata mechi mbili, ukiwarudisha tena uwanjani unaona viwango vyao vinakua vikubwa, msimu huu nimempa kila mchezaji nafasi ya kucheza, hata makipa wote watatu tumegawana mechi za kucheza," alisema Lukula.

Aliongeza ligi ya msimu huu bado ni ngumu na wamejipanga kuendelea kupambana kushinda kila mechi wanayocheza.

Katika mechi hiyo ya juzi, Mkenya Shikangwa alifikisha mabao 13 na kukaa kileleni baada ya kufunga magoli mawili, Vivian Corazone na Zainabu Mohamed, wakifunga pia.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PSG YAMSAKA KANE

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, 29, ndiye anayesakwa zaidi na Paris St-Germain msimu huu wa joto. ***(Le Parisien)***

### MOYES NJIA MOJA

KOCHA, David Moyes ana uwezekano mkubwa wa kuondoka West Ham ifikapo msimu huu wa joto huku mchakato wa kubaini watakaomrithi ukiendelea klabuni hapo. ***(Mail)***

### MIURINHO ANUKIA PSG

JOSE Mourinho anaweza kuwa kocha mpya wa Paris St-Germain msimu ujao huku bosi huyo wa AS Roma akiwa kileleni mwa orodha ya Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Luis Campos. ***(RMC Sport)***

### HODGSON KUBAKI PALACE

CRYSTAL Palace inataka, Roy Hodgson abaki katika klabu hiyo baada ya majira ya joto ili kumshauri yeyote atakayechukua nafasi yake kama kocha. ***(Telegraph)***

### GERRARD ANUKIA UGIRIKI

STEVEN Gerrard anaripotiwa kuwa kwenye orodha ya wanaotajwa kusaka nafasi ya kocha mkuu ajaye wa klabu ya Olympiakos ya Ugiriki miezi sita baada ya kutimuliwa na Aston Villa. ***(Express)***

### ALLISTER, ARSENAL BADO

MAZUNGUMZO kati ya Alexis Mac Allister, 25, ambaye ni nyota wa Brighton na mabosi wa Arsenal bado hayajafika popote. ***(Cesar Luis Merlo - via Twitter)***

### BARCA MATUMAINI KIBAO

BARCELONA inazidi kuamini mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina na Paris St-Germain, Lionel Messi, 35, atajiunga tena na klabu hiyo msimu wa joto. ***(Sport)***

### DE GEA, UNITED MAMBO SAFI

MANCHESTER United inakaribia kukubaliana mkataba mpya na mlinda mlango wa Hispania, David de Gea, 32, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

### JAMES AGOMBEWA ENGLAND

KLABU ya Southampton imemwambia kiungo, James Ward-Prowse, 28, anaweza kuondoka msimu wa joto ikiwa timu hiyo itashuka daraja. Tottenham Hotspur, West Ham na Newcastle United zote zinamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa England. ***(Sport)***

### AKHOMACH KUTUA LEEDS

LEEDS United itamsajili winga wa kimataifa wa Hispania, Ilias Akhomach, 19, baada ya kushindwa kukubaliana na Barcelona kuhusu kuongezwa mkataba. ***(Sport)***

### SANUSI ANUKIA UNITED

MASKAUTI wawili wa Manchester United walimtazama winga wa akademi ya Birmingham City na Timu ya Taifa ya England, Trevan Sanusi, mwenye umri wa miaka 15 siku ya Jumatatu. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LAMPARD: SIWEZI KULAUMU WACHEZAJI

### ●●● Ni baada ya kutolewa Ulaya huku nyota wake wakijipanga kuzinduka lala salama...

**LONDON,** England

FRANK Lampard ameapa "sitamweka yoyote katika ndoano" kwa Chelsea kutolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufungwa mabao 2-0 na Real Madrid katika mechi iliyochezwa juzi.

**Huo ulikuwa mchezo wa mkondo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwenye mchezo wa kwanza walifungwa idadi kama hiyo ya mabao walipocheza kwenye Uwanja wa Santiago Barnabeu wiki iliyopita.**

The Blues hao walipata kichapo cha nne mfululizo katika michezo mingi wakati Rodrygo alipofunga mara mbili na kwenye mchezo wa pili wa robo fainali ya michuano hiyo na kuwafanya Madrid kutinga nusu fainali kwa ushindi wa jumla ya mabao 4-0.

Kupoteza kwa Chelsea kunamaanisha Lampard amesimamia mwenendo mbaya zaidi wa klabu hiyo katika michuano yote kwa takriban miongo mitatu tangu arejee kama kocha wa muda.

Licha ya kichapo hicho kiungo huyo wa zamani alisema bado anahitaji kuona viwango vinapanda, na alisema hatamlaumu mchezaji yeyote kirahisi.

"Unachezea Chelsea," aliiambia BT Sport. "Kila mchezo unaocheza, lazima utoe kila kitu. Sitamlaumu mtu yeyote na lazima tuonyeshe kiwango. "Tulicheza vizuri sana kwa dakika 60. Tulitengeneza nafasi, lakini lazima uzichukue. Hutaki kusifia sana utendaji unapopoteza katika kiwango hiki.

"Lakini tulikuwa bora zaidi. Klabu hii imekuwa zaidi katika mashindano haya na wachezaji wanaweza kuchukua hisia hii mbele kwa siku zijazo."

Conor Gallagher aliunga mkono maneno ya kocha wake pia, akikiri Chelsea ilishindwa kutumia nafasi zao huku ukame wao wa mabao ukiendelea kuwatatiza. Akiwa amefunga mara moja tu tangu kuanza kwa Aprili, kiungo huyo wa kati wa England alisisitiza lazima wachukue matokeo chanya katika wiki za mwisho za msimu wa Ligi Kuu England.

"Soka ni kuhusu kuchukua nafasi zako, jambo ambalo hatukufanya leo (juzi)," aliongeza.

"Lakini hilo lilikuwa uboreshaji mkubwa kwenye maonyesho ya hivi majuzi. Tutaukubali mchezo mmoja baada ya mwingine. Tunatumai tunaweza kuendeleza uchezaji kwa sababu ninahisi ulikuwa mzuri kwa njia fulani."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,104,5

MECHI KALI

SEVILLA FC
VERSUS
MANCHESTER UTD

1 | 3.18
X | 3.38
2 | 2.13

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE GEA KITAELEWEKA MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano na David de Gea juu ya mkataba mpya, kwa mujibu wa ESPN.

Golikipa huyo anakaribia mwisho wa mkataba wake wa sasa na anaweza kuondoka Old Trafford bure mwishoni mwa msimu.


United, hata hivyo, wanaamini wako karibu na makubaliano ambayo yatamfanya De Gea kuongeza muda wake wa kukaa huku akipunguza mshahara wake wa kimsingi lakini kwa motisha kubwa inayohusiana na kiwango cha uchezaji.

Masharti mengi yamekamilika ingawa mazungumzo yanaendelea kuhusu jinsi mkataba huo ulivyopangwa.

United pia wana chaguo la kuweka nyongeza ya mwaka mmoja kwenye mkataba wake unaomalizika Mei, lakini kuna imani katika klabu masharti mapya yatakuwepo kabla ya hilo kuhitajika.

De Gea amekuwa namba moja muhimu kwa kocha, Erik ten Hag tangu kuwasili kwa Mholanzi huyo majira ya joto yaliyopita, na kucheza mechi 47 katika mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amecheza mechi zaidi ya 500 tangu alipowasili kutoka Atletico Madrid mwaka 2011.



## PSG yakomaa kumwania Kane

**PARIS,** Ufaransa

WAKATI mustakabali wa Harry Kane katika kikosi cha Tottenham Hotspurs haujulikani, huku mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2024 na sasa kuna ripoti matajiri wa jiji la Paris, Paris Saint-Germain imeonyesha nia ya kutaka kumsajili.

Kutokana na hali hiyo, uvumi unazidi kuibuka kuhusu kutakiwa kwa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England wakati wa dirisha la joto lijalo.

Manchester United wanajulikana kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, huku Bayern Munich pia hapo awali walihusishwa.

Na ripoti za hivi sasa zinesema Paris Saint-Germain wanawania kunasa saini ya mshambuliaji huyo, kwa mujibu wa gazeti la Le Parisien.

Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Luis Campos, anataka kuimarisha safu ya ushambuliaji na amemtambua Kane kama shabaha yao kuu.

Rais wa klabu hiyo ya Ufaransa, Nasser Al Khelaifi, ana uhusiano mzuri na Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, jambo ambalo linaweza kusaidia mazungumzo.

## HABARI MICHEZO


80,144/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/04/23 | 17:00 | Brentford FC vs Aston Villa | 2.41 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 22/04/23 | 17:00 | Leicester City vs Wolverhampton Wanderers | 2.38 | 3.15 | 2.85 |
| 03. 22/04/23 | 19:30 | Preston North End vs Blackburn Rovers | 2.46 | 3.20 | 2.70 |
| 04. 22/04/23 | 21:00 | FC Groningen vs NEC Nijmegen | 2.75 | 3.15 | 2.44 |
| 05. 22/04/23 | 21:45 | Sampdoria Genoa vs Spezia Calcio | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 06. 23/04/23 | 10:00 | Kawasaki Frontale vs Urawa Red Diamonds | 2.37 | 3.10 | 2.55 |
| 07. 23/04/23 | 13:30 | Kasimpasa Istanbul vs Konyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.35 |
| 08. 23/04/23 | 15:30 | PSV Eindhoven vs Ajax Amsterdam | 2.32 | 3.40 | 2.75 |
| 09. 23/04/23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs West Ham United | 2.85 | 3.15 | 2.39 |
| 10. 23/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs Stade Brest 29 | 2.95 | 3.00 | 2.42 |
| 11. 23/04/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.95 | 3.30 | 2.24 |
| 12. 23/04/23 | 18:30 | Brighton & Hove Albion vs Manchester United | 2.32 | 3.45 | 2.70 |
| 13. 23/04/23 | 18:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.55 | 3.40 | 2.49 |
| 14. 23/04/23 | 20:30 | Borussia Monchengladbach vs Union Berlin | 2.28 | 3.20 | 2.95 |
| 15. 23/04/23 | 21:45 | Juventus Turin vs SSC Napoli | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 16. 23/04/23 | 21:45 | Olympique Lyon vs Olympique Marseille | 2.37 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 23/04/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Villarreal CF | 2.85 | 3.25 | 2.34 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 20/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5798 | Leixoes SC U23 vs SC Farense U23 | 2.32 | 3.10 | 2.89 |
| 14:35 | 5967 | Wuhan Three Towns FC vs Beijing Guoan | 1.94 | 3.39 | 3.34 |
| 15:00 | 4356 | Ethiopian Medhin vs Mekelakeya | 2.10 | 3.37 | 3.06 |
| 17:00 | 3319 | SK Super Nova vs FC Riga | 21.74 | 7.45 | 1.09 |
| 17:00 | 4696 | Aegir vs Hafnarfjordur | 4.96 | 4.34 | 1.50 |
| 17:00 | 5449 | Ankaragucu vs Giresunspor | 1.90 | 3.57 | 3.57 |
| 18:00 | 1449 | Tigres U20 vs Puebla U20 | 1.50 | 4.06 | 5.04 |
| 18:00 | 2104 | Kari vs Thor Akureyri | 8.70 | 6.01 | 1.22 |
| 18:30 | 2014 | Be1 NFa vs FK Vilnus Bfa | 1.80 | 3.49 | 3.75 |
| 19:00 | 1430 | Shirak Gyumri vs Bkma Yerevan | 2.07 | 3.01 | 3.53 |
| 19:00 | 2360 | Sirens vs Pieta | 1.57 | 3.89 | 4.88 |
| 19:00 | 3615 | Naestved BK vs Vejle BK | 4.31 | 3.49 | 1.69 |
| 19:15 | 4038 | Pars Jonoubi Jam vs Esteghlal Mollasani | 2.06 | 2.85 | 3.78 |
| 19:45 | 4373 | Fiorentina vs Lech Poznan | 1.29 | 5.23 | 8.86 |
| 19:45 | 5466 | AZ Alkmaar vs Anderlecht | 1.73 | 3.63 | 4.44 |
| 20:00 | 1159 | Ahi Nazareth vs Hapoel Rishon Lezion | 2.53 | 3.18 | 2.70 |
| 20:00 | 1945 | Maccabi Petach Tikva vs El Fahem | 2.01 | 3.22 | 3.69 |
| 20:00 | 5581 | Hapoel Ramat Gan vs SC Kfar Qasem | 2.47 | 3.16 | 2.79 |
| 20:30 | 1989 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.74 | 3.16 | 2.48 |
| 21:30 | 5662 | Valletta vs Marsaxlokk FC | 1.83 | 3.42 | 3.84 |
| 21:45 | 1556 | Plymouth Parkway vs North Leigh FC | 1.48 | 4.46 | 4.98 |
| 21:45 | 1734 | Marske United FC vs Nantwich Town | 2.40 | 3.41 | 2.56 |
| 21:45 | 1774 | Alvechurch vs Royston Town | 1.97 | 3.78 | 3.06 |
| 21:45 | 3419 | Concord Rangers vs Dartford | 5.59 | 4.14 | 1.47 |
| 21:45 | 3826 | Tiverton Town vs Hayes Yeading United | 3.16 | 3.78 | 1.93 |
| 21:45 | 4282 | Metropolitan Police vs Bracknell Town | 3.42 | 3.73 | 1.85 |
| 21:45 | 4611 | Rushden and Diamonds vs Rushall Olympic | 4.66 | 3.99 | 1.58 |
| 22:00 | 3455 | Nice vs FC Basel | 1.52 | 4.12 | 5.62 |
| 22:00 | 3950 | Roma vs Feyenoord | 1.80 | 3.47 | 4.23 |
| 22:00 | 4162 | Sevilla FC vs Manchester Utd | 3.18 | 3.38 | 2.13 |
| 22:00 | 4896 | Union Saint Gilloise vs Bayer Leverkusen | 3.43 | 3.38 | 2.03 |
| 22:00 | 4967 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.25 | 3.17 | 3.12 |
| 22:00 | 5337 | West Ham vs KAA Gent | 1.63 | 3.73 | 5.04 |
| 22:15 | 1287 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.26 | 2.82 | 3.47 |
| 22:15 | 2226 | HK Kopavogs vs KFG | 1.14 | 6.99 | 12.34 |
| 22:15 | 2475 | Ceramica Cleopatra vs El Ittihad Alexandria | 2.21 | 3.06 | 3.27 |

IJUMAA - 21/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 2988 | Henan Jianye vs Qingdao Hainiu | 1.69 | 3.49 | 4.31 |
| 14:35 | 4003 | Chengdu Qianbao vs Shijiazhuang | 1.57 | 3.53 | 5.32 |
| 14:35 | 4523 | Shandong Luneng vs Nantong Zhiyun | 1.17 | 5.34 | 14.39 |
| 15:00 | 5469 | Kolos Kovalivka vs Zorya Lugansk | 3.55 | 3.40 | 1.87 |
| 21:00 | 2658 | Almere City vs PEC Zwolle | 3.33 | 3.54 | 1.95 |
| 21:00 | 3272 | FC Eindhoven vs NAC Breda | 2.03 | 3.43 | 3.22 |
| 21:45 | 1933 | Cork City vs Derry City | 4.11 | 3.39 | 1.75 |
| 21:45 | 2283 | St Patricks vs Shamrock Rovers | 3.40 | 3.35 | 1.94 |
| 21:45 | 4307 | Verona vs Bologna | 2.74 | 2.94 | 2.59 |
| 22:00 | 1492 | Espanyol vs Cadiz CF | 1.94 | 3.25 | 3.75 |
| 22:00 | 2826 | Angers vs Paris St Germain | 8.22 | 5.29 | 1.28 |
| 22:00 | 3225 | Eibar vs Zaragoza | 1.86 | 3.14 | 4.29 |
| 22:00 | 5946 | Arsenal vs Southampton | 1.21 | 5.73 | 11.64 |
| 22:15 | 4705 | Casa Pia Atletico vs Sporting Braga | 5.45 | 3.64 | 1.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MZFA YAMALIZA UTATA MABOSI TOTO AFRICANS

**Na Elias Kaswahili, SAUT**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Mwanza (MZFA), kimesema kinautambua uongozi wa Toto Africans FC ambao uliingia madarakani katika uchaguzi uliofanyika Aprili 8, mwaka huu na si vinginevyo.

**MZFA imetoa kauli hiyo kutokana na kuwapo kwa sintofahamu ya pande mbili za uongozi wa klabu hiyo kongwe hapa nchini.**

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa MZFA, Leonard Malongo, alisema chama hicho kinautambua uongozi unaoongozwa na Mwenyekiti, Gasper MwanaLyela, kwa sababu ndio ulifanyika kwa kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa.

Malongo alisema, pia wanaitambua Kamati ya Uchaguzi iliyosimamia uchaguzi wa klabu hiyo ambayo ni mwanachama wa MZFA.

Aliongeza MZFA haiutambui uongozi mwingine wa Toto Africans ambao ulichaguliwa Aprili 14, mwaka huu na endapo wataendelea kujitangaza, watawapeleka katika Kamati ya Maadili ili kuchukuliwa hatua.

"Sisi kama viongozi wa MZFA hatuutambui uchaguzi huo, zaidi ya ule uliofanyika tarehe 8, mwezi huu. Uchaguzi ambao mamlaka za mpira na za kiusalama zinautambua pamoja na viongozi wote walioshiriki katika uchaguzi huo mwingine watapelekwa katika Kamati ya Maadili kujieleza," alisema Malongo.

Aliwataja viongozi wengine wa Toto Africans wanaowatambua ni pamoja na Juma Mrisho ambaye ni Makamu Mwenyekiti huku wajumbe wa Kamati ya Utendaji ni Saleh Akida, Hussein Tade, Yusuph Budodi na Kenneth Shuma.

Inaelezwa viongozi waliomaliza muda wao waliendesha uchaguzi mwingine Aprili 14, mwaka huu ambao Rajab Mbalamwezi, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti, Martha Haule (Makamu Mwenyekiti), Chassa Mongella (Katibu) na wajumbe ni Karim Mushi, Beatus Madenge, Ismael Ismael, Daud Mkama na Yusuph Kisena.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia ( wa pili kulia), akifurahia jambo na wadau wa michezo katika futari iliyoandaliwa na shirikisho hilo kwenye Kituo cha Michezo cha Mnyanjani kilichoko jijini, Tanga jana. **PICHA: TFF**

## Simba: Tunataka heshima tena

INATOKA UK. 24

ga kwenye Uwanja wa Uhuru, tukaenda kumtoa kwao, heshima ya mnyama, ikaandikwa Afrika. Miaka mingi imepita sasa, bado tuna heshima ya 2003, lakini muda umefika ya kuandika heshima mpya, nayo ni kumtoa Wydad Casablanca na kwenda nusu fainali, Wanasimba wote wanaamini inawezekana," alisema Ahmed.

Wydad Casablanca imetua na msafara wa watu zaidi ya 50, ambao ni wachezaji, benchi la ufundi, viongozi na baadhi ya mashabiki.

Beki wa kati ya timu hiyo ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Arsene Zola, mara baada ya kuwasili alisema wamekuja kupambana kupata matokeo mazuri kwa ajili ya kurahisisha kazi kuelekea mechi ya marudiano.

Hata hivyo Zola alikiri mechi hiyo ya keshokutwa haitakuwa rahisi.

"Itakuwa mechi nzuri na ngumu, sisi tumekuja kutafuta matokeo mazuri, tunajua Raja Casablaca walishinda mabao 3-0, lakini siyo kama wao walishinda basi na sisi itakuwa rahisi hivyo, hizi ni mechi mbili tofauti, naifahamu Simba ni timu nzuri na kubwa Afrika, nawafahamu wachezaji Wakongo wenzangu, Henock Inonga, na yule Jean Baleke ni mdogo wangu nilikuwa naye TP Mazembe," alisema Zola.

## *Viungo Yanga wamvuruga*

INATOKA UKURASA 24

"Jumapili tutacheza mchezo mkubwa na muhimu katika historia yetu, mpinzani anapokuja uwanja wa nyumbani hasa kwa Mkapa, tunapata matokeo mazuri, sasa katika hatua hii usipocheza vizuri ugenini basi itakuwa ngumu kushinda nyumbani.

Hatutaki kuwa na wakati mgumu nyumbani kurudisha mabao matano, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Rivers United wanapokuwa kwao ni timu ngumu na tishio sana kutokana na kutumia vyema uwanja wao, lazima tupambane kushinda mechi ya ugenini ambayo tutacheza," alisema Kamwe.

# Michezo

Alhamisi Aprili 20, 2023
Nipashe



'Siwezi kulaumu wachezaji' UKURASA 21



Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, akizungumza katika uzinduzi rasmi wa tawi la klabu hiyo la Wekundu wa Chalinze uliofanyika mkoani, Pwani jana. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba SC: Tunataka heshima tena CAF

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Wydad Casablanca kutoka Morocco ikiwa imewasili salama katika ardhi ya Tanzania, Simba imetamba iko tayari na kamili kurudia ilichokifanya mwaka 2003 kwa kuwavua taji waliokuwa mabingwa wa Afrika, Zamalek ya Misri, imeelezwa.

Simba itawakaribisha mabingwa watetezi, Wydad katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi rasmi wa Tawi la Wekundu wa Chalinze, Pwani, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya miaka 20, imefika wakati timu yao ikaweka rekodi nyingine ya kuwavua ubingwa Wydad kama walivyofanya mwaka 2003.

"Tuna shughuli moja tu ya kwenda kumnyoa Wydad Casablaca ili tuandike historia nyingine ya kumvua mtu ubingwa. Tunajua mechi ni ngumu, tunacheza na mtu aliyetudizi viwango vya CAF, tunacheza na mabingwa watetezi, lakini Wanasimba tukiunganisha nguvu na kushikamana, Wydad Casablaca hawana pa kutokea.

Inaonekana ni kama ndoto ya mchana hivi tukizungumzia kuifunga, siku zote sisi tunazungumza kile ambacho tunachokiweza kwa sababu tumeshawahi kufanya hivyo huko nyuma," alisema Ahmed.

Aliongeza hata mwaka 2003 hakuna aliyeamini kama Simba inaweza kuwafunga Zamalek, na hata iliposhinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), watu hawakuamini kama wanakwenda kupata matokeo mazuri ugenini, badala yake kila mmoja alidhani itafungwa mabao mengi.

"Tumeshawahi kufanya hivyo, kwa hiyo tunazungumza tunachokiweza, tulipangiwa Zamalek, wakiwa wa moto kweli kweli lakini tukasimama imara tukamfun-

INAENDELEA UKURASA 23

# Viungo Yanga wamvuruga Nabi

## Awaandalia 'darasa' maalum ili kuimaliza Rivers United ugenini na...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga inaondoka leo kuelekea Nigeria, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, amesema amelazimika kuandaa programu maalum ya kuwanoa viungo wake ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi ya hatua ya robo fainali dhidi ya wenyeji, Rivers United itakayochezwa Jumapili nchini humo.

**Akizungumza na Nipashe jana, Nabi, alisema hakufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na viungo wake katika mchezo dhidi ya Simba hali iliyomlazimu 'kukaa chini' na kuandaa 'darasa' kabla ya kuwavaa Rivers United katika mchezo wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Nabi alisema kutofanya vyema kwa viungo wake kulipelekea kwa kiasi kikubwa kupoteza mechi hiyo ambayo ilikuwa muhimu kwenye kampeni ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambao bado wanalishikilia.

Kocha huyo alisema anaamini kuimarika kwa viungo wake kutasaidia katika mechi hiyo ya kwanza ambayo wanahitaji kushinda na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Aliongeza hakupendezwa na namna safu hiyo ilivyocheza katika mchezo huo lakini anaamini watajirekebisha na kurejea kwenye ubora wao kabla ya kuwakabili Rivers United.

Alisema pia ukiondoa hilo, kikosi kipo vizuri na maandalizi yao kuelekea mchezo huo wa Jumapili yako katika hatua za mwisho huku wakiahidi kufanyia kazi makosa yote yaliyojitokeza katika mechi iliyopita.

"Safu ya kiungo ilikuwa chini sana tofauti na nyakati nyingine, hali iliyopelekea kupata matokeo mabaya upande wetu, hii imetufanya tuweke mikakati na programu mpya ambayo itahusisha pia washambuliaji kwa ajili ya mchezo wetu ujao.

Najua tuna mchezo mgumu sana mbele yetu, malengo yetu ni kuona tunapata matokeo mazuri na kurejea katika hali yetu ya siku zote, kila mchezaji anatambua majukumu yake na anaweza kuyatimiza maana tunachokiangalia ni uwezekano wa kushinda ugenini," alisema Nabi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema hawajamaliza kazi waliyonayo katika msimu huu kutokana na malengo waliyokuwa nayo.

Kamwe alitaja bado malengo yao ni kutwaa mataji yote (Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA -ASFC) na kufanya vizuri katika mechi ya CAF.

"Mipango yetu msimu huu ni kubeba makombe, kila Mwanayanga anataka kuiona timu yake ikibeba Kombe la Ligi, Kombe la FA na ubingwa Afrika, huu utakuwa mwezi wa mapigano makubwa katika kutimiza malengo yetu, vyakula vyote vizuri bado viko juu ya meza yetu, tushikane wananchi," alisema Kamwe.

Aliongeza kikosi cha timu yao kitaindoka nchini leo saa 12:00 afajiri na ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia, halafu wataweka kambi fupi ya siku moja jijini Lagos na Jumamosi wataelekea katika kitongoji cha Omagwa, sehemu utakaochezwa mchezo huo.

Alisema wanakwenda Nigeria kucheza mechi kubwa na malengo yao ni kupambana kusaka ushindi ili kurahisiha kazi kwenye mchezo wa nyumbani na hatimaye kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >